Gazeti la kwanza la Kiislam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Haji ni miezi maalum: na anayekusudia kufanya Haji katika (miezi) hiyo, basi asiingiliane wala asitukane wala asibishane katika Haji; na heri yoyote mnayoifanya, Allah Huijua; na chukueni masurufu, na hakika masurufu bora ni ucha Mungu, na Nicheni Mimi enyi wenye akili. (2:198)

JUZU 75 No. 186 | DHUL QA'DAH 1437 AH | AGOSTI 2016 | ZAHOOR 1394 HS | BEI TSH. 500/=

Khalifa Mtukufu aongea na viongozi wa Jumuiya:

Itumikieni Jumuiya kwa unyenyekevu

Na Mwandishi wetu
Dar es Salaam

Muhtasari wa Hotuba ya Hadhrat Khalifatul Masih V (Kiongozi wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya duniani) a.t.b.a. katika Sala ya Ijumaa ya 3 Juni 2016.

Baada ya Salamu, *Tashahhud*, *Taaudh* na kusoma *Suratul Faatiha*, Huzur Aqdas a.t.b.a. alisema:

Muda fulani uliopita, niliwahi kueleza jambo hili katika moja ya hotuba zangu kwamba mwaka huu ni wa uchaguzi wa viongozi wa ofisi mbalimbali ndani ya Jumuiya (Ahmadiyya Muslim Jamaat). Chaguzi hizo zimeshafanyika katika maeneo mengi katika ngazi ya kitaifa na katika ngazi za matawi. Viongozi wapya wa ofisi mbalimbali wameshaanza kutekeleza majukumu yao.

HadhratMasroor Ahmad, Khalifatul Masih V a.t.b.a.

Wakati ambapo katika baadhi ya maeneo viongozi waliochaguliwa kushika ofisi katika ngazi ya kitaifa au ya matawi ni wapya, katika maeneo mengi viongozi waliokuwemo kwenye uongozi uliopita wamechaguliwa tena.

Kwa wale ambao wamechaguliwa kushika ofisi kwa mara ya kwanza hawana budi kumshukuru Allah kwamba wao wamechaguliwa kuitumikia Jumuiya na kwa ajili ya hilo lazima watafute msaada wa Allah wakipiga magoti mbele yake kwa unyenyekevu kwamba Allah amewapatia nafasi na hivyo wairudishe amana waliyokabidhiwa kwa kutekeleza wajibu wao.

Na kwa namna hiyo hiyo, viongozi ambao wamechaguliwa kwa mara nyingine lazima pia wamshukuru Allah kwa kuendelea kuwapatia nafasi ya kumtumikia tena na lazima waombe kwa unyenyekevu kwamba Allah Awawezeshe kutekeleza majukumu ya amana waliyopewa kwa uwezo wao wote. Allah, kwa fadhili zake, ameyafumbia macho mapungufu, uvivu na uzembe waliofanya ambao bila shaka uliwazuia kutekeleza mahitaji ya majukumu yao, na kwamba, kwa neema yake, nafasi aliyowapatia ya kuitumikia tena Jumuiya kwa miaka mitatu ijayo isiathirike kutokana na uvivu, upungufu na uzembe, na kwamba Allah awawezeshe kutekeleza majukumu ya amana waliyoaminiwa kama inavyotakiwa.

Ni lazima izingatiwe kwamba kuihudumia Jumuiya hakupaswi kuchukuliwa kuwa jambo dogo na haipaswi kuchukuliwa kijuu juu tu. Kila mmoja wetu, awe ni kiongozi wa ofisi au mwanajumuiya wa kawaida, ameahidi kutoa

Endelea uk. 3

Mahafali Jamia Ahmadiyya yafana

Sheikh Abid Mahmood Bhatti, Principal Jamia Ahmadiyya, Tanzania.

Kwa msaada wa Allah Aliye msaidizi wetu mkuu, chuo chetu cha ualim (***Jamia Ahmadiyya***) kilichopo Kihonda katika Mkoa wa Morogoro kimefanya mahafali yake ya kuwaaga walimu wa mwaka huu mnamo tarehe 26/07/2016 siku ya Jumanne. Sherehe hizo zilifanyika katika ukumbi wa chuo uliopo katika eneo hilo.

Mgeni rasmi katika hafla hiyo alikuwa ni Amir na Mbashiri mkuu wa Jumuiya ya Waislam Waahmadiyya Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry sahib.

Hafla ilianza saa 5:00 asubuhi chini ya Mwenyekiti Sheikh Abid Mahmood Bhatti sahib mkuu wa chuo. Taratibu za

Picha ya pamoja Amir na Mbashiri Mkluu, Uongozi na walimu pamoja na wanafunzi wa Jamia Ahmadiyya Morogoro waliohitimu masomo yao mwaka 2016

Mahafali hayo yalikua kama hivi ifuatavyo:-

Usomaji wa Qur`an Tukufu ulisomwa na Mwl. Mzee Muhammad Mzee. Kisha lilifuata shiri la Kiurdu ambalo lilisomwa na Mwl. Bashirud-din Ramadhan. Baada ya usomaji wa shairi, ilifuata taarifa ya mwaka ya chuo ambayo ilisomwa na Sheikh Azizi Ahmad Shahzad sahib. Katika taarifa yake sheikh Azizi sahib alisema, kwa fadhila za Allah na kwa dua maalum za Hadhrat Khalifatul Masih V a.t.b.a mwaka wa chuo 2015/2016 umekamilika kwa mafanikio makubwa katika sekta mbalimbali – Alhamdulillah.

Msomaji aliwakumbusha

Endelea uk. 2

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

HIJJA NI ISHARA YA UMOJA

Kuhiji huko Kaaba ni nguzo ya Tano ya Islam. Hija inakusudiwa kuingiza ndani ya nyoyo za waaminio umuhimu wa nguvu ya pamoja katika lengo la kuwaunganisha wanadamu, katika kupambana na tabia mbaya ya kuiangukia dunia na ladha zake na hatimae katika kufikia mapenzi ya kweli ya Allah. Hilo ndilo lengo kuu la Hijja.

Dhana hii ya kuhiji inaonekana takribana kwenye dini nyingi, lakini Islam inao upekee katika hili kwamba kuna sehemu moja tu ya kufanya hija ambayo ni Makka, ambapo waislamu, duniani kote, hutakiwa kukusanyika kwa ajili ya Allah tu. Mamilioni ya Waislamu kutoka mataifa mbalimbali, yenye rangi mbalimbali, lugha mbali mbali na tamaduni na makabila mbalimbali hukusanyika Makka mara moja kwa mwaka kwenye ibada ya Hija, tukio ambalo hudhihirisha udugu wa kidunia kwa namna ambayo haiwezi kuonekana kwenye dini yoyote iwayo.

Watu walianza ibada hii ya Hija tangu enzi za Nabii Ibrahim lakini baadae muanguko ukatokea na Ibada hii ikabaki kuwa ushirikina na ujahili mtupu. Inasemwa kwamba ilifikia mahala ikaamuliwa kwamba ni Makuraishi ambao ndio kabila tukufu wangeweza kuzunguka Kaaba wakiwa wamejifunika shuka au nguo fulani, lakini makabila mengine yote yalitakiwa kuzunguka wakiwa uchi. Hivyo kwa ujio wa Mtukufu Mtume s.a.w. ibada hii ikarejeshwa kwenye uasili wake, ujahili na ushirikina ukaondolewa bali ikafanywa kuwa nzuri zaidi kwa kuongezwa baadhi ya mambo muhimu sawa na zama zake.

Hija ni ibada ambayo mtu analazimika kuifanya mara moja maishani mwake iwapo atakuwa na uwezo wa kufanya hivyo.

Hija hufanywa kwenye siku maalum kuanzia mwezi 8 Dhul-Hijjah, ambao ni mwezi wa 12 wa kalenda ya kimwezi ya Kiislam, hadi 12 au 13 ya mwezi huo huo. Kuna matendo mengi ambayo hufanyika wakati wa Hijja, lakini ni muhimu yote yakachukuliwa yenye kuashiria hekima na falsafa fulani ya ndani ya kiroho badala ya kuchukuliwa kuwa ni mambo ya dhahiri tu.

Mambo hayo ni pamoja na Ihram ambayo ni kuvaa shuka nyeupe zisizoshonwa na bila kufunika kichwa kwa wanaume na kutokujifunika uso kwa wanawake. Katika Ihram mahujaji hawaruhusiwi, kupunguza nywele, kukata kucha, kujipaka manukato, kuwinda, kukutana kimapenzi mtu na mke wake ikimaanisha kwamba ni ishara ya kuyauwa matamanio yote ya dunia, usawa wa wanadamu, kukumbushia maisha yajayo na kuanza na moyo safi katika safari ya kumwendea Mungu.

Mara baada ya kuvaa Ihram Hujaji hutakiwa kuanza kusoma Talbiyyah: ***Labaika Allahumma Labaika*** .....

Wakiwa wamevaa Ihram mahujaji huelekea Kaaba kwa lengo la kufanya Tawafu ya kuwasili, Tawaf-e-Qudum,

Hujaji huanza Tawaf yake mahala penye jiwe jeusi lisilo chongwa (lisilo na sura maalum) huku wakisoma Talbiyya kwa moyo wote. Ni vyema ifahamike kwamba hakuna ibada ifanywayo kwa ajili ya jiwe hilo jeusi kama wadhanivyo baadhi ya wapinzani wa Islam. Jiwe jeusi inasemwa ndilo jiwe lililobaki kutoka kwenye ujenzi wa Nabii Ibrahim na mwanawe Ismil. ambao walijenga kwa mawe, likiashiria umoja wa Allah kwa kutokuchongwa kwake.

Matukio mengine ya Hija ni Kusai (kukimbia baina ya safa na Marwa), ikiashiria tukio la Bibi Hajira kukimbia baina ya vilima hivyo wakati alipokuwa akihangaika kumtafutia maji mtoto wake mchanga.

Siku ya 8 Dhul Hijjah. wakiwa kwenye Ihram mahujaji huelekea Mina. Hapo Mina mahujaji hutakiwa kutumia muda wao wote kwa ajili ya kumkubmuka Allah na kumuomba.

Siku inayofata 9 Dhul Hijjah, ambayo ndiyo huitwa hasa siku ya hija, mara baada ya sala ya Alfajiri wanatoka Mina kuelekea viwanja vya Arafat. Hapo Arafa kama maana ya neno lilivyo ni utambuzi wa kina, mahujaji wanatarjiwa wapate kumtambua au wapate maarifa zaidi ya Allah na sifa zake na utukufu wake.

Mahujaji hukaa hapo hadi mchana na husali Adhuhuri na Alasiri na kabla ya kusali Magharibi huondoka kueleka Muzdalifah – maana yake ni kuwa karibu zaidi. Ikimaanisha hapa hujaji hutakiwa kuwa karibu zaidi ya Allah au kupata maarifa ya kumtambua Allah.

Kutoka Muzdalifa siku ya mwezi 10 Dhulhijaa mahujaji baada ya kusali alfajiri huelekea tema Mina. Hapo pana nguzo 3 ambazo mahujaji hutupa vijiwe kwa idadi maalum kama ishara ya kumfukuza shetani. Kwenye siku hiyo ya 10th Dhul Hijjah, baada ya kurusha vijiwe kwenye Jamrah 'Aqabah mahujaji huchija wanyama wao wa dhabihu na baadae wananyoa, huoga na kuvaa nguo zao za kawaida.

Kwa ujumla Hija ni ibada ambayo inazo falsafa nyingi na faida nyingi, ambazo zinatakiwa ziwe sehemu ya maisha ya waislamu baada ya kutekeleza nguzo hiyo, ingawaje kwa bahati mbaya leo hatuzikuti ndani ya maisha ya waislamu na hata wale waliowahi kuhiji. Hii ndio moja ya sababu ya kutumwa kwa Masihi Aliyeahidiwa a.s. ili kuja kuturejesha kwenye kiini cha Ibada ya Hija.

Mahafali Jamia Ahmadiyya yafana

Kutoka uk. 1

wanachuo na wageni waalikwa historia fupi na iliyotukuka ya idara hii muhimu ya Jamia Ahmadiyya akisema hii ni idara iliyoanzishwa na Imamu wa zama hizi – yaani Hadhrat Masihi Mauud a.s. na kuendelea kusimamiwa kwa karibu na makhalifa wake watukufu katika nyakati zote.

Aliendelea kusema kuwa chuo cha Jamia Ahmadiyya sio tu kinawahimiza kushindana katika medani ya kiakili, kimwili na kiroho, bali pia kinawahimiza kushindana katika kuonyesha khulka njema katika maisha yao ya kila siku.

Alisema kwa upande wa taaluma, wanafunzi hufundishwa masomo mbalimbali kama vile:-

Tajweed, Tafsiri ya Qur`an Tukufu pamoja na maelezo yake, Hadithi za mtume saw, Fiqhi, Sira na historia, kalaam (kujenga hoja), Kiarabu, Kiurdu, Kiingereza, n.k.

Msemaji aliendelea kusema kuwa mbali na masomo ya darasani pia wanachuo huingizwa katika mpango wa mashindano ya taaluma (kielimu) kama vile usomaji wa Qur`an Tukufu, usomaji wa mashairi, kutoa adhana, kuhifadhi dua za Qur`an pamoja na za mtume saw, utoaji wa hotuba, n.k. ili kuinua na kuboresha viwango vya elimu na uelewa kwa ujumla.

Ili kujenga na kuimarisha afya za wanachuo, chuo huwashindanisha katika mshindano ya kimwili kama vile, mpira wa miguu, mpira wa meza, mpira wa wavu, riadha (mbio ndefu na fupi) kuruka nk. Aliendelea kusema kuwa, ili kuboresha hali ya kielimu na kimwili, wanachuo toka asubuhi hadi jioni hushiriki katika mipango mbalimbali kama vile masomo, michezo, muda wa kujisomea, nk.

MAHUBIRI:

Taarifa hiyo imeonyesha kuwa kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi wanachuo pamoya na walimu wao hufanya makhubiri. Zaidi ya vipeperushi 1200 vimegawiwa, watu zaidi ya 36000 wamefikiwa na ujumbe na vitabu vyenye thamani ya Tsh. 300,000/= vimeuzwa.

WAQAR-E-AMAL:

Wanachuo pia wanashiriki katika kazi za kujitolea yaani waqar-e-amal na jumla ya waqar –e-amal 260 zimefanyika na masaa 2200 yalitumika na kuokoa kiasi zaidi ya Tsh.4,960,000/=

Pia wanachuo pamoja na walimu wao wamejitolea michango nk. Na jumla ya Tsh.11,273,950/= zimetolewa katika mpango huo na watu wapatao 675 wamesaidiwa. Mbali na ratiba ya chuo, wanafunzi pia wameshiriki katika shughuli mbalimbali za makao makuu kama vile Jalsa Salana, mkutano wa Shuraa, Ijitimaai ya khuddam na pia wanachuo wameshiriki katika maadhimisho ya siku muhimu za Jamaat kama vile siku ya Mwana Aliyeahidiwa, siku ya Masihi Aliyeahidiwa, siku ya Ukhalifa, Seeratunnabiyy nk.

MIRADI MIPYA:

Msemaji aliendelea kusema kuwa, kwa fadhili za Allah chuo kimefanikiwa kufanya miradi mipya kadhaa kama vile:-

Ujenzi wa madarasa mapya, uandishi wa makala za kielim kwa wanafunzi wanaomaliza, pia kupata mwanafunzi wa kwanza aliyemaliza kuhifadhi Qur`an Tukufu yote, na kuanzisha darasa la kompyuta.

Kwa ajili ya kutekeleza agizo la Khalifa mtukufu a.t.b.a wanachuo pamoja na waalimu walikuwa wakifunga saumu ya nafali kila siku ya Alhamisi sambamba na kutoa dhabihu kila mwezi. Kuongeza mashindano mapya ya kutoa hutuba katika lugha za Kiarabu Kiurdu na Kingereza. Kupanga siku maalum ya michezo yaani 'Sports day' ambapo timu tatu (3) za AMANAT, SHAFQAT, na SHUJA`AT, zilipambana vilivyo na washindi kupatikana.

Kufuatia agizo la Amir Jamaat, zaidi ya nusu ya wanachuo pamoja na waalimu wawili walikwenda katika mikoa ya Shinyanga na Simuyu katika mpango wa WAQF E ARZI; mpango huu umeleta mafanikio mazuri katika swala zima la malezi kwa wanajumuiya wapya waliopatikana huko.

Baada ya usomaji wa riport hiyo, Mwenyekiti wa hafla hiyo ambae pia ni mkuu wa chuo Sheikh Abid Mahmood Bhatti alimkaribisha mgeni rasmi ambaye ni Amiri na mbashiri mkuu wa Jumuiya hapa nchini Sheikh Tahir Mahmood Chaudhiry sahib ili akabidhi zawadi kwa washindi wa mashindano mbalimbali pamoja na wale walioshika nafasi mbalimbali pamoja na wale walioshika nafasi za kwanza katika mitihani. Zawadi pia zilikabidhiwa kwa waalimu wa Jamia, wafanyakazi mbalimbali wa Jamia, wabashiri wa Mkoa wa Morgoro, Dodoma nk.

Baada ya kazi hiyo kukamilika, mwenyekiti wa hafla hiyo alitoa maelezo machache na kumkaribisha mgeni rasmi Ili atoe nasaha kwa wahitimu, wanachuo na wageni waalikwa.

Katika nasaha zake, Amiri Sahib alisema na kusisitiza juu ya suala zima la kufuata mafundisho ya Qur`an Tukufu, mafundisho ya Mtume mtukufu s.a.w, mafundisho ya Masihi Aliyeahidiwa a.s pamoja na makhalifa wake. Amiri sahib alisisitiza kusikiliza maelezo ya khalifa wa zama a.t.b.a na kuyafanyia kazi.

Pia Amiri sahib aliwaeleza wasikilizaji juu ya maendeleo mazuri ya masomo kwa vijana wa kitanzania wanaosoma katika chuo cha ubashiri huko Ghana na kuwataka wanachuo waongeze bidii zaidi katika masomo yao na kamwe wasipoteze muda katika mambo yasiyofaa. Aliwaeleza wahitimu kuwa wao ni mabalozi huko watakako pangiwa, hivyo wahakikishe kuwa wanawakilisha vyema Jamati kwa kuonyesha khulka njema zitakazokuwa kivutio kwa jamii jambo ambalo litawarahisishia utendaji wa majukumu yao ya kila siku katika jumuiya.

Mwisho Amiri sahib aliwaombea kheri na baraka nyingi wote waliohudhulia katika hafla hiyo, kisha aliongoza maombi ya kimya na kufunga kikao. Baada ya hapo wote walipiga picha pamoja na Amir sahib. Kisha mwenyekiti wa hafla aliwakaribisha wageni waalikwa katika chakula cha pamoja ambacho kiliandaliwa baada ya sala ya Adhuhuri na Alasiri.

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Mahmood Hamsin Mubiru.
Kompyuta: Abdurahman M. Ame.
Mchapishaji: Sheikh Muhammad Arif
Msambazaji: Omar Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Abdullah Khamis Mbanga
2. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu@yahoo.com

Itumikieni Jumuiya kwa unyenyekevu

Kutoka uk. 1

kipaumbele juu ya maswala ya imani kuliko ya kidunia. Wakati mtu anakubali kuhudumu kama kiongozi, au kwa ajili ya huduma maalum, yeye ana wajibu zaidi kuliko wengine wa kutimiza ahadi yake na kukumbuka kwamba yeye amefanya ahadi hii na Allah, na kwamba Allah ametuelekeza katika maeneo mengi ndani ya Qurani Tukufu kutimiza ahadi. Hivyo, kumbukeni daima kwamba Allah waziwazi amesema kuwa amana ambayo umepewa na ukakubali kuipokea, basi hiyo ni ahadi yako na hivyo mnapaswa kutimiza amana zenu na ahadi zenu.

Katika sehemu moja Allah ametaja ishara hii ya watu ambao ni wakweli katika kauli yao na wanaotembea juu ya njia ya haki;

... Na wale watekelezao ahadi zao wanapoahidi ... (2:178)

Hii inapaswa kuwa tofauti bayana hasa kwa wale watu ambao wameshika nafasi za uongozi ndani ya Jumuiya kwamba wanao wajibu wa kutimiza majukumu yao kwa kudumu juu ya ukweli na kuinua viwango vyao vya taqwa. Iwapo kutakuwa na mashaka mashaka yoyote katika kiwango chao cha ukweli, kama kutakuwa na mapungufu, kama kiwango chao cha taqwa sio mfano kwa wanajumuiya wa kawaida basi hao watakuwa hawajatimiza ahadi yao, pia watakuwa hawajatimiza majukumu ya ofisi zao na imani yao. Maamiri na Marais lazima wawe wa kwanza kuonesha mifano yao bora mbele ya kamati kuu za utendaji (Majlis Amilas) na mbele ya wanajumuiya wa kawaida.

Kuna makatibu wa malezi, wamepewa jukumu la kusimamia kazi ya malezi, ila mafunzo ya malezi wanayotoa yanaweza tu kukamilika wakati ambapo mifano yao bora itakuwa ni imara. Mtu ambaye ni mfanyakazi, ambaye ni mwenye wajibu fulani, ambaye anawashauri wengine, lazima mwenyewe awe ni mwenye kutekeleza maelekezo kwa matendo. Makatibu wa malezi wanapaswa kuonyesha mifano bora mbele ya wanajumuiya kwani majukumu ya kuwalea wengine ndani ya Jumuiya yako juu yao.

Nimeshawahi kutaja mara kadhaa kwamba iwapo idara ya malezi inakuwa hai kazi za idara nyingi zingine zitajitimiza zenyewe. Kwa kukua kwa kiwango cha malezi miongoni mwa wanajamaat, kazi za idara zingine zinakuwa rahisi. Kwa mfano kazi za katibu wa fedha zitakuwa rahisi, kazi za katibu wa mambo ya ndani zitakuwa rahisi, hivyo hivyo kwa kazi za makatibu wengine, kazi za Bodi ya Qadha (Ofisi ya Kadhi) nazo pia zitarahisika.

Mimi kwa kawaida husema kuwa katika mikutano ya Majlis Amila katika maeneo mbalimbali waanze kazi ya malezi kutoka majumbani mwako. Nyumba hii haitakiwi iwe ya katibu wa malezi tu badala yake nyumba ya kila mjumbe wa Majlis Amila inatakiwa iwe ni kituo cha malezi. Wajumbe wa Majlis Amila wanatakiwa wote, wawe mbele katika kujilea wenyewe. Mipango yoyote ambayo Maamiri, Marais au Makatibu wa malezi wanaipanga, wanapaswa kwanza kuielekeza kwa wajumbe wa Majlis Amila na kuona iwapo wanaitekeleza mipango hiyo au la.

Je wajumbe wa Majlis Amila wanatimiza maamrisho ya msingi ya Allah na madhumuni ya kuumbwa kwa mwanadamu? Kama si hivyo basi hakuna uchamungu.

Ibada ni miongoni mwa haki kubwa za Allah. Wanajumuiya wanaume wanaelekezwa kusimamisha sala mwisho wa uwezo wao. Kusimamisha sala maana yake ni kusali katika jamaa. Hivyo Maamiri, Marais, na viongozi wa osifi wanapaswa kufanya juhudi za pamoja za kuhakikisha kwamba wanasimamisa sala, tena kwa jamaa. Matokeo yake misikiti yetu itajaa, vituo vya Sala navyo vitajaa, watakaoijaza misikiti na vituo hivyo nao watajikusanyia baraka za Allah, na kwa mfano wa matendo yao bora, watakuwa ni sababu ya mafunzo ya kimalezi kwa wanajumuiya wengine, na watakuwa warithi wa Baraka za Allah, na kazi zao zitafanywa kuwa rahisi zaidi. Wao watakuwa si watu wa maneno matupu tu.

Hivyo, viongozi lazima kwanza wajichunguze wenyewe kwamba kwa kiasi gani maneno yao na vitendo vyao vinawiana. Allah anasema,

Enyi mlioamini! mbona mnasema msiyoyatenda? (61:3)

Masihi Aliyeahidiwa, amani iwe juu yake anasema:

Aya hii inasema kwamba katika ulimwengu kulikuwa, na bado wataendelea kuwepo wale ambao wanasema lakini hawafanyi sawa na wanayoyasema wenyewe. Kumbukeni ninachokisema na kizingatieni daima kwamba kama maneno ya mtu hayatoki kwa moyo wa kweli na hakuna nguvu ya matendo inayofuatana na maneno hayo, basi hayawezi kuleta athari zake. Kumbukeni kwamba, ufasaha wa maneno ya hotuba tu hauwezi kuwa na maana mpaka utakapoongozana na utendaji. Maneno tu hayana thamani yoyote mbele ya Allah.

Masihi Aliyeahidiwa a.s. kwa mnasaba wa amri hii ya Allah ameeleza wazi kwamba ni lazima kusiwepo mgongano baina ya maneno na matendo. Wasimamizi wetu wa ofisi hawana budi wajitathmini wenyewe, wakiyaweka maagizo haya mbele yao.

Sala zinaweza kuandaliwa majumbani pale ambapo masafa ni makubwa au pale ambapo kuna nyumba chache tu na hapana huduma ya msikiti wala kituo cha sala. Kiuhalisia hilo si jambo gumu. Wanajumuiya wengi wanajitahidi kulitekeleza. Ingawaje hawana jukumu maalum walilopangiwa, na wala sio wajumbe wa Majlis Amila yoyote, lakini wanawakusanya wanajumuiya majumbani mwao na wanasimamisha sala ya jamaa. Iwapo kuna umakini, kila kitu kinawezekana. Kila Kiongozi awe makini juu ya kusimamisha sala kwa jamaa, vinginevyo watakuwa hawatimizi haki ya amana waliyopewa. Quran tukufu imelitaja jambo hili kwa namna mbalimbali.

Viongozi wa Jumuiya daima waliweke jambo hili mbele ya macho yao kwamba Allah amelitaja hili kuwa ni ishara ya waaminio wakweli kwamba wanazingatia amana zao na majukumu yao na wanayalinda hayo. Wanajitahidi kwamba yasiwepo mapungufu au uzembe kutoka upande wao kuhusiana na amana waliyokabidhiwa na viapo walivyofanya vya kuihudumia Jamaat, kwani hilo si jambo dogo.

Allah amesema pia katika Quran tukufu:

Na timizeni ahadi. Kwa hakika ahadi itaulizwa. (17:35).

Ibada ndio jambo la msingi na ndilo lengo la kuubwa kwa mwanadamu. Ni lazima tulitekelezee haki yake. Hakutakiwi kuwe na uzembe juu ya hili kwa upande wa viongozi, bali kwa hakika juu ya kila mwaminio.

Kuna mambo mengine vilevile ambayo ni lazima yatekelezwe na viongozi wa Jamaat. Mambo hayo yanahusiana na haki za wanaohudumu maofisini na tabia zao mbele ya wanajumuiya. Mambo haya pia yanahusiana na viapo au majukumu ya washika ofisi. Hakuna kiongozi anayeteuliwa kutoa huduma kwa lengo la kuwa afisa tu, badala yake katika Islam dhana ya kuwa mhudumu/mshikilia ofisi inayo maana tofauti kabisa.

Mtukufu Mtume s.a.w. amelieleza hili pia.

Alisema: Kiongozi wa watu ndie mtumishi wao.

Kwa kiongozi wa ofisi kutimiza majukumu ya amana aliyokabidhiwa huku akiwaheshimu watu ni kulitumikia taifa. Hali hii huzalika ndani ya mtu iwapo anao moyo wa kujitolea ndani mwake. Anakuwa mnyenyekevu na mpole. Kiwango chake cha uvumilivu kinakuwa cha hali ya juu hata kuwashinda wengine. Baadhi ya nyakati viongozi inawabidi kusikia maneno yanayowalaumu. Lakini ikibidi kuyasikiliza ni lazima wayasikilize. Viongozi wanaweza wao wenyewe kujitathmini ni kwa kiwango gani wanavumilia na kwa kiwango gani ni wenye unyenyekevu.

Baadhi ya nyakati taarifa zinapatikana kwamba baadhi ya viongozi hawana uvumilivu kabisa, na inapokuwa upande wa pili nao hauna subira basi huzidi kuwa wakali. Iwapo mwanajumiya wa kawaida hana subira, haileti tofauti yoyote kwake. Itasemwa tu kwamba hana tabia nzuri. Lakini iwapo maneno yasiyostahiki yanatoka kinywani mwa kiongozi, yanaathiri hadhi na heshima ya kiongozi huyo, bali na wanajumuiya wengine pia. Kiwango ambacho Jumuiya inabidi iwe nacho, na kiwango ambacho Masihi Aliyeahidiwa a.s. alitarajia atuone tumekifikia ni kwamba hata mfano mmoja wa namna hiyo usipatikane mahala popote kwani ukipatikana utakuwa ni fedheha kwa Jumuiya. Lakini tunapata kuona mifano hiyo katika baadhi ya seheme. Malumbano huweza kuanza hata misikitini. Mambo kama hayo huwaathiri vibaya mno watoto na vijana.

Ni nini Allah anakitarajia kutoka kwetu, na ni vipi Allah amemtaja yule anayesimamisha viwango vya kujitoa mhanga nafsi yake? Mahala fulani anasema.

Na wanawapendelea kuliko nafsi zao ... (59:10).

Mfano huu ulionyeshwa na Maansari (wenyeji wa Madina) kwa Muhajirina (wahamiaji kutoka Makka). Na huu ni mfano kwetu. Kumpendelea mwingine dhidi ya nafsi yako ni daraja la juu zaidi na ni ustadi mkubwa. Wakati mwingine hata haki za mtu zinakuwa hazitimizwi vya kutosha. Baadhi ya mambo huwa yanafikishwa kwa viongozi au baadhi ya mambo yanatoka makao makuu ya kimataifa yakihitaji uchunguzi, lakini taarifa huwa zinatengenezwa kwa kizembe sana. Taarifa huwa inatumwa bila ya kulichunguza suala kwa umakini. Au, jambo linacheleweshwa sana kiasi kwamba kama mtu ana haja inayopaswa kutimizwa, basi haja haitekelezwi au anavumilia kwa shida. Baadhi ya viongozi huwa wanatoa udhuru wa kuwa na shughuli nyingi. Wengine hawana hata udhuru wowote. Ni kutokujali tu. Kama ni suala linalowahusu wao wenyewe au suala linalowahusu jamaa zao, basi kipaumbele kinakuwa tofauti. Hamu ya kutoa huduma ya kweli, hamu ya kujitolea muhanga, kutekeleza haki ya ulichoaminiwa kwa ukamilifu ni kuwa mwenye msaada kwa mwingine huku ukiwa na wasiwasi kama umemtekelezea kikamilifu. Kama huduma inatolewa kwa moyo wa kiwakfu, na kuona matatizo ya mwingine kuwa ni yako, basi kiwango cha kujitolea cha wanajumuiya kitaongezeka. Muelekeo utakuwa ni wa kutimiza haki na wala si kuzinyang'anya. Tunasema mbele ya wengine kwamba amani inaweza kudumishwa duniani ikiwa katika kila ngazi endapo, badala ya kujihakikishia haki zetu sisi wenyewe na kutotoa haki za wengine, hamu ya kuhakikisha haki za wengine na hamu ya kujitoa wakfu inazalika. Kama hatuna kiwango hiki miongoni mwetu basi tutakuwa tunafanya kitu ambacho Allah Hakipendi.

Khulka ambayo viongozi lazima wawe nayo ni upole. Allah ameutaja huu kuwa ni dalili ya watumishi wa Mwingi wa Rehema.

Na watumishi wa Rahmani ni wale wanaotembea ardhini kwa unyenyekevu (25:64)

Viongozi wetu ni lazima wawe na mfano mkubwa wa upole ndani yao. Kadiri ofisi inavyokuwa ni ya ngazi ya juu zaidi upole lazima uwe mkubwa zaidi utakaoonyeshwa na hamu ya kutoa huduma unapokutana na watu. Hivi ndivyo kuwa mwenye adhama. Watu wanaona na kuhisi jinsi gani tabia za viongozi zilivyo. Wakati mwingine watu wananiandikia pia kwamba hiyo ndiyo ilikuwa tabia ya kiongozi fulani lakini nilifarijika sana leo kwamba kiongozi huyo sio tu kuwa alinisalimia lakini pia aliniuliza kuhusiana na hali yangu na alinipokea kwa khulka njema na nilifurahi kuona tabia yake na adhama yake iliyoonyeshwa na tabia yake.

Wengi miongoni mwa wanajumuiya wanakuwa na utayari kwa kila jambo la kujitolea wakiwa wameridhishwa na upendo, upole na tabia njema. Kama kuna aina yoyote ya kujiona mkubwa au maringo kwenye

Endelea uk. 4

Itumikieni Jumuiya kwa unyenyekevu

Kutoka uk. 3

moyo wa kiongozi, basi atambue kwamba inamuweka mbali na Allah. Pale mtu anapokuwa mbali na Allah, hakuna Baraka zinazobaki katika kazi zake. Kazi ya imani ni kwa ajili ya kupata radhi ya Allah tu, na kama hakuna Radhi ya Allah basi mtu wa aina hiyo anakuwa ndio chanzo cha kuharibu Jumuiya badala ya kuwa ni chanzo cha kuleta faida. Viongozi ni lazima daima wawe wanajitathmini katika suala hili kama wana upole au hawana, na kama wanao basi je ni wa kiwango gani. Mtume Mtukufu (saw) alisema kwamba kadiri mtu anavyoshika upole zaidi na zaidi ndivyo Allah Anavyompa cheo cha juu zaidi na zaidi kulingana na kiwango chake. Kila kiongozi ni lazima akumbuke kwamba kama Allah Amempa fursa ya kuitumikia Jamaat, ni Upendeleo wa Allah na kushukuru upendeleo huo ni kukuza upole zaidi na unyenyekevu Kwake.

Kama upole na unyenyekevu hauongezeki basi hakuna shukurani kwa Allah inayotendeka.
Inaonekana kwamba baadhi ya watu wakikutana katika hali za kawaida wanaonyesha upole wa hali ya juu. Wanawapokea watu kwa adabu zinazostahili. Lakini kunapotokea utofauti wa maoni na mtu aliye chini yake au mtu wa kawaida hapo sasa tabia zao rasmi zinaamka na wanaonyesha tabia za ukubwa na majivuno mbele ya yule mtu aliye chini yake. Upole sio kwamba uwe unaonyeshwa pale penye makubaliano na kwamba hakuna kupinga. Upole wa aina hii ni wa bandia. Ukweli unaibuka pale inapokuwepo tofauti ya maoni au mfanyakazi anaposema dhidi ya madhanio basi hapo uamuzi ufanywe baada ya kutathmini maoni yaliyotolewa kwa kina huku ukisimama thabiti katika haki. Kwa upole wa aina hii, moyo adhimu pia utaonekana. Kama itakuwa hivyo basi upole huo utafahamika kuwa ni upole wa ukweli. Kiongozi ni lazima daima azingatie agizo hili la Allah:
Na wala usigeuze shavu lako mbali na watu kwa maringo na wala usitembee ardhini kwa majivuno (31:19)

Nimetaja utofauti wa maoni. Ningelisema hili kuhusiana na jambo hili kwamba ingawa kanuni zinamruhusu Amiri kwamba baadhi ya wakati anaweza kukataa maoni ya Majlis Amila na akaamua sawa na anavyoona yeye lakini daima jitihada lazima ifanyike kwamba mtu aendane na kila mtu na maamuzi yafanyike na kazi ifanyike kwa mashauri na kwa maoni ya wengi. Katika maeneo fulani, Amiri anaanza kuitumia haki hiyo zaidi bila ya ulazima. Haki hii itumike katika hali ambapo ni lazima sana kwamba itumike ambapo inaonekana kuwa Jumuiya itapata hasara na kuna masuala ambayo yanahitaji kufafanuliwa kwa wajumbe wa Majlis Amila. Kwenda kinyume na maamuzi ya wengi katika Majlis Amila lazima kufanyike kwa kuzingatia manufaa makubwa ya Jumuiya. Kwa hili msaada wa Allah lazima utafutwe kwa maombi. Usitegemee maamuzi yako pekee. Lazima ieleweke kuwa haki hii si kwa ajili ya Maraisi wa nchi au marais wa matawi kwamba wakatae maoni ya Majlis na kwamba waamue sawa na waonavyo wao.

Ili kuelewa mipaka ya haki za mtu, ni muhimu kwa viongozi kusoma na kuelewa sharia na kanuni. Kama watazifuata sheria na kanuni basi mambo madogo madogo hayatakuwa yenye kuhitaji wajumbe wa Majlis au wanajumuiya kwa ujumla.

Sifa nyingine ya viongozi ni lazima iwe kwamba wawatendee walio chini yao kwa upendeleo. Kazi nyingi za Jumuiya ni za kujitolea. Wanajumuiya wanajitolea muda. Wanajitolea muda kwa ajili ya kazi za Jumuiya ili kupata radhi ya Allah. Wanajitolea muda kwa sababu wana uhusiano na mapenzi kwa Jamaat. Viongozi lazima waziangalie hisia za walio chini yao na wawatendee kwa upendeleo. Hili hasa ni Agizo la Allah. Kwa upendeleo huu, jitihada zifanyike kuwapa mafunzo walio chini yao na wasaidizi ili mfanyakazi awe tayari daima kuendesha kazi za Jamaat. Allah anaendesha kazi za Jamaat, hakuna shaka, lakini kama viongozi wenye uzoefu wakaandaa safu ya pili ya wafanyakazi, watapata Baraka ya jitihada hii pia. Kwa Baraka za Allah si mimi wala si makhalifa walionitangulia walikuwa wanajua ni jinsi gani kazi ya Jumuiya itakavyofanyika. Hii ni Ahadi ya Allah kwa Masihi Aliyeahidiwa (as). Ataendelea kuleta wafanyakazi waaminifu.

Ofisa mmoja wakati wa Khalifa wa tatu (ra) wa Masihi Aliyeahidiwa (as) alidhani kwamba mfumo wa kifedha wa Jamaat unafanya kazi kwa kupendeza kutokana na kazi na jitihada yake. Khalifa wa tatu (ra) alipojua, alimteua mtu kwa ajili ya kazi hii ambaye alikuwa hajui hata kidogo elimu ya uhasibu. Kwa kuwa hii ni kazi ya Allah, na kwa sababu ya ulinzi maalum kwa Khalifa wa Allah, Baraka nyingi mno zikaja kwenye kazi ya mtu mpya kiasi kwamba hakuna kama hizo hata zingeweza kuwazwa kabla ya hapo. Kwa hiyo, viongozi wanapewa fursa na Allah. Allah anatoa fursa kwa wafanyakazi wa Jumuiya; kwa hiyo, lisiwepo hili katika moyo wa mtu yeyote kuwa uzeoefu wake au elimu yake ndiyo inayofanya au inayoweza kufanya kazi ya Jumuiya isonge mbele. Ni Baraka za Allah tu ndizo zinazofanya kazi ya Jumuiya. Udhaifu wetu mwingi na mapungufu ni kwamba kama ingekuwa ni kazi ya kidunia, kusingekuwa na Baraka yoyote, wala matokeo mazuri yasingepatikana, lakini Allah Anajaziliza na Yeye Mwenyewe Anasaidia na Malaika Wake. Kwa kutolea mfano, kwa kazi ndogondogo za kila siku za Ulaya, Allah Ametoa aina ile ya wafanyakazi ambao wamekulia hukuhuku katika nchi hizi, ambao wamejitafutia elimu wao wenyewe na kisha wanawajibu wapinzani kwa namna ambayo inamshangaza mtu. Wapo wengi vijana wa aina hiyo ambao kutokana na majibu yao ya aina hiyo wapinzani wanakuwa hawana njia ila kukimbia. Hivyo viongozi waichukulie fursa ya kufanya kazi kuwa ni upendleo wa Allah na wala si kwa uzoefu wao, utaalamu au uwezo.

Sifa bainifu nyingine ambayo viongozi lazima wawe nayo ni ucheshi na tabia njema. Allah Anasema:
….. na mseme na watu kwa wema (2:84)

Yaani, shughulika na watu na zungumza nao kwa upole na tabia njema. Hii pia ni khulka ya msingi ambayo ni lazima iwepo kwa wingi miongoni mwa viongozi. Khulka adhimu lazima zionyeshwe kila mara unapozungumza na walio chini yako, wafanyakazi wenzako na wengine. Kwa ajili ya masuala ya kiratibu wakati mwingine inabidi kujieleza kwa uimara lakini ulazima wa kufanya hivyo iwe ni njia ya mwisho. Kama mtu akishauriwa kwa upendo na viongozi wakiwa wanajua kwamba hao ni wanaowatakia kheri basi asilimia 99 ya watu ni wa aina hii ya kwamba wataelewa na watakuwa tayari kushirikiana na Jumuiya kwa sababu wana uhusiano na Jumuiya. Sharti kubwa kabisa na la muhimu ni kwamba hisia hii ijengeke miongoni mwa watu au watu wajenge hisia kwamba viongozi ni wenye manufaa kwao. Zungumza kwa upole na watu. Likifanyika kosa usibane kiasi hiki kwamba mwanzoni mtu anakuwa hapati mwanya wa kujieleza. Lakini wale ambao ndio tabia yao, na wanarudia mara kwa mara, na wanajaribu kuleta mkorogano na msuguano katika kila jambo, wanapaswa kushughulikiwa ipasavyo lakini lazima kuwe na uchunguzi kamili katika hali za aina hii. Kumshughulikia ipasavyo kusipelekee kwenye chuki binafsi bali kuwe kwa ajili ya kurekebisha. Wakati fulani Mtume (saw) alimshauri Gavana wa Yemen, jenga hali ya tahfifu kwa watu sio shida, sambaza upendo na furaha, usiruhusu uadui kumea.

Huu ni ushauri ambao unaleta uzuri katika mahusiano kati ya viongozi na wanajumuiya. Matokeo yake, hisia za kuthaminiana zinajengeka miongoni mwa wanajumuiya vilevile.

Hivyo viongozi (wajumbe wa Majlis Amila) wana wajibu mkubwa, na hasa Maamiri, maraisi, idara za mafunzo na taasisi zinazotoa hukumu kwamba watafakari njia zinazoleta tahfifu kwa watu. Lazima itiliwe maanani kwamba njia hizi zifuatwe lakini mkiwa ndani ya mipaka ya Amri za Allah, na sio kama watu wa kidunia kwamba tusahau Amri za Allah ili kuwapa watu tahfifu. Kwa kuzingatia mipaka ya Sharia, kwa kuzingatia Radhi ya Allah Taala, lazima tutoe haki za watu na lazima tulinde viapo vyetu na amana.

Kama nilivyosema kila mwanajumuiya lazima aviangalie vitabu vya sharia na kanuni na ajipatie elimu ya majukumu ya idara zao. Kila mmoja aijue mipaka yake.

Wakati mwingine viongozi wala hawajui mipaka yao. Idara moja inafanya shughuli wakati shughuli hizo zimeorodheshwa kwenye idara nyingine. Wakati mwingine tofauti kati ya shughuli za idara moja na nyingine haziko bayana sana kiasi kwamba isipofikiriwa kwa umakini itatokea idara mbili zinaingiliana katika majukumu. Hivi majuzi nilikuwa na kikao na Majlis Amila ya Uingereza. Pale nilihisi kwamba kutokana na kutoelewa hizi tofauti zisizo wazi sana mjadala usio wa lazima ukaanza. Kama tungesoma kanuni wakati ule basi muda usingepotea kwa namna hiyo. Kwa mfano, idara ya Tabligh ifanye shughuli za Tabligh na pia ifanye mawasiliano. Tabligh itapanuka kwa kufanya mawasiliano. Umur Kharijiyya lazima nao pia wafanye mawasiliano na pia waitambulishe Jamaat. Mduara wa majukumu yao hauingiliani. Moja inafanya hivyo kwa madhumuni ya Tabligh na nyingine inafanya hivyo kwa madhumuni ya Mahusiano na umma, kuongeza mahusiano. Lengo hasa ni kuitambilisha Jumuiya na kuitambulisha imani ili kwa kuwaleta watu kwa Allah tunajaribu kunyoosha mwisho wao na pia kuonya kuhusu hali ya amani duniani. Lengo letu sio kupata sifa za kidunia, lengo hasa ni kumridhisha Allah na kupata Radhi yake. Kama idara zitafanya kazi kwa kushirikiana matokeo yake yatakuwa mazuri zaidi kwa kiasi kikubwa.

Kutoka sehemu nyingi, hili linaonekana pia kwamba bajeti za idara mbalimbali hazipangwi sawasawa. Bajeti iliyopitishwa na Shuura itolewe na Katibu anayehusika awe na udhibiti wa matumizi ya bajeti hiyo. Ni lazima ya kwamba Katibu auwakilishe mpango wa kazi wa mwaka mzima kwenye Majlis Amila na matumizi yanayoendana na mpango ulioidhinishwa na kazi iwe inafanyiwa tathmini katika kila kikao cha Majlis Amila. Kama kutakuwa na haja ya kubadilisha mpango wa kazi au bajeti yake au kama kuna fursa ya kuifanya iwe nzuri zaidi basi hiyo iangaliwe tena upya.

Hili pia ni jukumu muhimu la Maamiri na Maraisi na Makatibu kwamba wawe wanatekeleza na wahakikishe wametekeleza kikamilifu na kwa haraka kwa kuzingatia kwa ukamilifu sekula na maagizo yanayopokelewa kutoka Makao makuu. Malalamiko yanakuja kuhusu baadhi ya Jamaat kwamba maagizo ya Makao Makuu hayatekelezwi ipasavyo. Ikiwa kwa sababu ya hali ya nchi au tawi, jambo lina vizuizi, hata hivyo haraka sana ombi lifanywe ili mabadiliko yafanyike katika mahitajio yaliyomo kwenye agizo; hili ni jukumu la Amiri au Raisi/Sadr. Halitakuwa jambo sahihi hata kidogo kwamba kwa kutumia maoni yake, agizo linawekwa pembeni na kuachwa na halitekelezwi na wala Makao Makuu haijulishwi.

Ufidhuli wowote wa aina hiyo utakaofanywa na Amiri au Raisi yeyote utachukuliwa kuwa ni kuiambaa Makao Makuu na Makao Makuu inaweza kuchukua hatua kuhusiana na hilo.
Kuhusiana na watu waliomo kwenye mpango wa Wasia, jambo la kwanza ninalotaka kusema ni kwamba ni wajibu wa kila Muusi kufanya malipo kwa kudumu na kutunza kumbukumbu zake za malipo ya michango lakini ni jukumu la Ofisi ya kimataifa na makatibu wahusika kuhakikisha kwamba wanatunza kumbukumbu kamili ya kila mwana Wasia na kuwakumbusha inapokuwepo haja kuhusiana na hali ya hesabu zao. Ni jukumu la Makatibu wa Taifa kuwahamasisha makatibu wa matawi kwamba wawe na mawasiliano na kila mwana Wasia. Imeonekana baadhi ya wakati kwamba kuhusiana na masuala fulani wakati ripoti inahitajika ya mtu na mtu huyo ni mwana Wasia, inaelezwa kwamba

Endelea uk. 7

Ahmadiyyat Mkoani Kagera

Na Mahmood Hamsin Mubiru.

Historia ya Ahmadiyya kandokando ya ziwa Lweru (ambalo kwa makosa na kwa sababu ya ukoloni linaitwa Victoria) ni ya kusisimua mno. Ili kuifaidi hasa inahitajika utafiti wa kina. Sikumbuki hata kidogo mapambano ya kalamu miaka ya 60 kama yale yaliyojitokeza baina ya Masheikh wa Kishia wakiongozwa na Sheikh Idrisa Byakutaga kwa upande mmoja na upande mwingine alikuwepo yule jemedari mahiri Maulana Sheikh Muhammad Munawwar Chaudhry aliyekuwa Amir na Mbashiri Mkuu wa Jumuiyya ya Ahmadiyya Tanzania. Kagera nzima ilikuwa katika kizaazaa kikubwa. Yalikuwa ni mapambano makali na ya kisomi yaliyopata mashabiki wengi khususan wanafunzi wa shule ya Nyakato.

Vijana hao wa Nyakato waliovutiwa na hoja zilizokuwa zinatolewa na Sheikh Muhammad Munawwar na vitabu alivyokuwa anarejea, lakini kupita yote elimu yake ya Qurani Tukufu vyote hivyo viliwagusa mno vijana hao wa shule ya Nyakato. Ni desturi ya wasomi siku zote kutaka kufanya utafiti na kudadisi. Vijana hao walifanya hivyo kwa kupeleleza habari za Ahmadiyya kwa Masheikh ambao wote walibaki vinywa wazi wasiwe na njia yoyote ya kutetea msimamo wao. Hali ya kutokuwepo majibu ya kutosha kuondoa kiu yao, ikawafanya vijana hao kuchukua uamuzi mgumu wa kujiunga na Jumuiyya ya Ahmadiyya. Hatua hiyo ilikuwa ngumu na tunaweza kuinasibisha na kusaga pilipili na kuiweka kwenye kidonda. Walizomewa, wakabezwa, wakatukanwa. Vijana hao hata hivyo walisimama imara katika imani yao. Hao ni pamoja na Jenerali Twaha Khalfan Ulimwengu, Ahmad Kiwanuka na Issa Zakaria.

Jenerali Twaha Khalfan Ulimwengu ambaye baadae alikuwa Katibu wa Vijana wa Afrika huko Algers – Algeria, mwandishi wa magazeti ya Daily News, Mkuu wa wilaya ya Ilala na Mwandishi na mmiliki wa vyombo vya habari, alipata msukosuko mkubwa. Wazee mashuhuri wa wa Bukoba Mjini akiwemo Mzee Sefu Mchanandevu, walimwita kwenye kikao maalum ili aachane na Ahmadiyya. Jenerali aliitikia na akawaambia ya kwamba kinachotakiwa ni wao kujenga hoja ya kuonesha kwanini Waahmadiyya wamepotea. Kikao hicho kilishindwa kutoa hoja yoyote na kwa hasira wakampa taarifa baba yake kwamba mwanao amepotea. Baba yake mzazi Khalfan Ulimwengu alikasirika sana na kutoa vitisho vingi. Kitisho cha mwisho ni watu wa Bukoba Mjini kubeba jeneza wakiwa wanasema wanakwenda kumzika Jenerali. Vitisho hivyo havikumyumbisha hata kidogo. Masheikh hao wa Bukoba walikuwa na desturi siku ya Idi kukodi gari na watoto wote wa Kiislam kugawanywa katika familia za Kiislam ili kusherehekea Idi. Jenerali na wenzake wawili Ahmad na Issa waliambiwa kwamba sawa na itikadi ya Masheikh hao, wao hawakuwa Waislam na hivyo wakaachwa pale shuleni wakati wenzao wanakwenda kusherehekea idi.

Kijana wa pili aliyesimama imara licha ya vitisho ni Ahmad Kiwanuka. Yeye aliathirika sana na mafundisho ya Ahmadiyya na watu wawili walimvutia sana katika Jamaat. Hao ni Sir Muhammad Zafrullah Khan na Sheikh Kaluta Amri Abedi. Zilikuwa ni siku za mapenzi makubwa kwa Jamaat hata jina lake alilibadili ili liwe kama la Sheikh Amri. Hivyo akawa K. Ahmad Ayubu. Alikuwa Mhubiri mzuri aliyetembelea vijiji vingi akieleza ujaji wa Masihi wa Mtukufu Mtume Muhammad (saw). Makala zake zilitokea katika Mapenzi ya Mungu na alitunga mashairi ya kuonesha kuwa katu hawezi kuacha haki. Moja ya mashairi yake matamu ni hili lilitokea katika Mapenzi ya Mungu mwezi Machi 1966. Alilolipa anuwani 'Katu sitoacha haki'.

Enyi ndugu wa Bukoba salaam nawatolea
Japo mwaniita simba, baidi kunikimbia
Nataka mjue kwamba, haki sitoiachia
Kamwe sitoacha haki, japo mnanichukia.

Waniita Qadiani, hata kafiri tambua
Siwakindi asilani, zidini kunizomea
Atapotaka Manani, wenyewe tajijutia
Kamwe sitoacha haki, japo mnanichukia.

Wengine mwanitangaza, jina kuniharibia
Vijijini mnawaza, sifa mtajizolea
Kadamnasi mwaanza, Kiwanuka kafiria
Kamwe sitoacha haki, japo mnanichukia.

Kiwanuka aliandika makala nyingi za kuitetea imani yake. Ushahidi tunaupata katika makala aliyoipa anuani 'Ukweli wa Ahmadiyya' na makala haya yalitoka katika gazeti la Mapenzi ya Mungu la mwaka 1965 uk. 3. Mwisho mwa makala hayo anaandika; "Na hao ndio watakao stawi. Hapo kustawi kwenyewe ndiko kupanuka kwa Jumuiyya, kuwa na watu wengi na kufanya kazi kwa wingi. Upanukaji ndio ule uenezaji wa Jumuiyya. Ahmadiyya sasa ipo katika kila nchi ya ulimwengu. Huku kwetu ilianzia Tabora sasa Ahmadiyya ipo pote Afrika ya Mashariki. Wale wanaoichukia Ahmadiyya hawataweza kuishinda, bali wao wafanye hima katika kujiunga na Ahmadiyya tu".

K. Ahmad Ayubu alipopata habari za ujaji wa Masihi Aliyeahidiwa aliniandikia barua niende makao makuu ya Jumuiyya ya Ahmadiyya kwani palikuwa na vitabu na magazeti na alikuwa anafahamu fika juu ya mapenzi yangu ya vitabu na magazeti. Kutokana na barua hiyo ya K. Ahmad Ayubu mwishoni mwa Disemba 1965 niliingia Masjid Salaam, na toka wakati huo Alhamdulillah bado nimo katika nyumba hii ya Salama.

Issa Zakaria alipata mgogoro kwani ndugu zake walikuwa wasomi wasomi wa mambo ya dini. Hata hivyo hoja zao hazikufua dafu mbele ya hoja madhubuti za Ahmadiyya.

Miongoni mwa Mashiekh wa mwanzoni mwanzoni kutembelea Kagera alikuwa Sheikh Inayatullah Ahmad ambaye alitembelea sehemu nyingi za Bukoba. Lakini Masheikh waliokaa kwa muda mrefu ni Sheikh Hafidh Suleiman na Sheikh Yusuf A. Kambaulaya. Sheikh Hafidh Suleiman alifanya kazi ya kusambaza vitabu na magazeti. Kila Jumapili alitembelea magereza kuwahubiri wafungwa. Tukio la simanzi na majonzi lilikuwa ni wakati ule ambapo Sheikh Hafidh Suleiman alifiwa na mwanae na watu wa Bukoba walikosa kumsaidia katika kuzika na ikabidi amzike yeye peke yake.

Sheikh Yusuf A. Kambaulaya alifanikiwa kuzitembelea sehemu nyingi za Kagera kueneza vitabu, kuwa na mijadala na kusambaza vipeperushi. Alihakikisha kwamba amepiga hodi katika Ofisi zote na kuwafikishia ujumbe wa Masihi Aliyeahidiwa (as). Itakumbukwa kuwa Sheikh Yusuf Kambaulaya alikuwa anaitumikia Mwanza pia. Baadae tutaweza kuona shughuli za Masheikh hao wawili tutakapotizama kwa undani Jumuiyya ya Ahmadiyya Katoma kilomita chache kutoka Bukoba Mjini.

Unapozungumzia Jumuiyya ya Ahmadiyya Katoma, bila kuweka chumvi unazungumzia kimsingi kazi kubwa aliyoifanya Bw. Abdallah Bishazo Rutashongerwa katika kueneza mafundisho ya Ahmadiyya. Tunaelewa kuwa historia ya mahala popote haitengenezwi na mtu mmoja, lakini ni dhahiri kuwa wapo wenye mchango mkubwa wa kihistoria kuliko wengine. Bwana Abdallah Bishazo amepanda mbegu na matunda yake yanaliwa pande zote za Kagera na nje ya mipaka ya Tanzania. Ni ukweli usiopingika ya kwamba Jumuiyya ya Rwanda inakiri kuwa waanzilishi wa Jumuiyya hiyo huko ambako sasa wamejenga Msikiti walikuwa ni vijana wawili Bw. Adam Kahamile na Bw. Idrisa Sengoga waliohubiriwa juu ya Ahmadiyya na Bw. Abdallah Bishazo. Wanahistoria watakumbuka ya kwamba katika miaka ya 60 kulitokea machafuko ya kisiasa nchini Rwanda yaliyosababisha vifo na kupatikana kwa wakimbizi wengi. Kama zilivyo nchi nyingi za kiafrika siasa zinatawaliwa na ukabila. Sera maalum iliyoletwa na wakoloni ya wagawe uwatawale. Uhasama wa kikabila umekuwa na athari kubwa sana katika mambo ya kisiasa na kijamii katika sehemu nyingi za Afrika kama tulivyotangulia kusema. Vyama vya siasa nchini Rwanda vilijengwa kwenye misingi ya Ukabila. Hilo lilikuwa ni bomu lililokuwa linasubiri kulipuka. Nchini Rwanda yapo makabila makuu matatu. Kihistoria Batutsi walikuwa wanajiita "National ad imperium" (bora) na kuwaona Bahtu kama "facti ad servitum" (watumishi) na Batwa walidharauliwa na makundi hayo mawili. Wakati wa vuguvugu la kisiasa katika miaka ya 50 na 60 vilianzishwa vyama vya siasa vyenye muelekeo wa kikabila mathalan Union Nationale Rwandaise kilianzishwa na Francois Ruheba kikiungwa mkono na Mfalme Kigeri–V na kikataka uhuru kwanza. Chama hiki kiliungwa mkono na wanamapinduzi wa Afrika wakiwemo Ghamal Abdul Naser, Kwame Nkurumah, Patrice Lumumba, Sekoture na Modibo Keita. Chama kingine kilikuwa Parmehtu (Chama cha ukombozi wa Wahutu) kilichoanzishwa na Gregoire Kayibanda wao walisema wanapigania haki za Wahutu na kupinga ukoloni wa Watusi. Chama kingine kilikuwa ni Aprosoma (Chama cha maendeleo ya Uma) kilichoongozwa na Joseph Giteza na chama cha Radel kilichoongozwa na Prosper Bwanakweli. Hawa walitaka Demokrasia kwanza.

Ni bayana vyama hivyo vya siasa havikuwa na dira moja. Kuna chama kilichosema wakoloni ni Watusi, kuna kilichosema kwamba kabla ya uhuru ilitakiwa Demokrasia. Kwa ufupi palikuwepo na kutoaminiana. Hali hiyo mwaka 1960 iliileta maafa makubwa na watu wakakimbia kutoka Rwanda kwenda Congo ndio hao wanaoitwa Wanyamurenge na wengine walikuja Bukoba bado vijana wadogo na ndio hao vijana waliohubiriwa na Bw. Abdallah Bishazo na hatimaye wakajiunga na Jumuiyya ya Ahmadiyya.

Ni vizuri tumfahamu Bwana aliyewahubiri vijana hao kutoka Rwanda. Bw. Abdallah Bishazo. Bw. Abdallah Bishazo alizaliwa mwaka 1908 kijiji cha Igombe. Kazi yake ilikuwa ni ya biashara. Kufanikisha biashara zake aliona ni vyema kuwa karibu na mji wa Bukoba. Hivyo alihama kutoka Igombe hadi kijiji cha Mauguru kilichomo katika kata ya Katoma na akaishi na mjomba wake aliyekuwa Sheikh jina lake Athumani. Hapo ndipo aliposilimu na kupata elimu nzuri ya dini ya Islam. Alijifunza Qurani Tukufu na tafsiri yake. Hivyo ujumbe wa Ahmadiyya ulipokuja Bwana huyo shujaa na asiyekata tamaa alijiunga bila ya hofu. Tumeambiwa tuwe na majina mazuri. Bishazo ni jina zuri linaloambatana na khulka ya Bw. Abdallah Bishazo. Kama tulivyokwisha sema Bw. Bishazo alikuwa ni mfanyabiashara lakini pia alikuwa mwindaji. Wawindaji wakitoka mawindoni wanapewa pole kwa kuambiwa "Shwaga" na kama mtu hakuambulia chochote husema "Nimeambulia Bishazo" (Majani yanayochoma). Hata hivyo hurudi kesho yake bila kukata tamaa. Kwa kutumia neno hilo mara kwa mara akapata jina Bishazo. Ni vigumu kuelewa hasa alijiunga lini katika Jumuiyya ya Ahmadiyya. Bw. Abdu Bishazo anaeleza kuwa alikuwa anatumwa mara kwa mara kwa Sheikh Hafidh Suleiman ili kumletea gazeti la Mapenzi ya Mungu. Bw. Abdu Bishazo anakumbuka kwamba Sheikh Hafidh Suleiman alikuwa anampa gazeti la Mapenzi ya Mungu – gazeti linalotoka mara moja kila mwezi. Bw. Abdallah Bishazo hakukubali kukosa gazeti hilo hivyo kila mwisho wa mwezi Abdu Bishazo alifunga safari kutoka Katoma hadi kwenye shirika la nyumba za taifa karibu na machinjioni alikokuwa anaishi Sheikh Hafidh Suleiman. Hapo ndipo alipomkuta Sheikh Hafidh Suleiman mpole na mwenye tabasamu na humpatia gazeti la Mapenzi ya Mungu.

Kutoka kwa Sheikh Hafidh Suleiman akiwa na gazeti la Mapenzi ya Mungu mkononi bw. Abdu Abdallah alipita pale Nyangoye ambapo kuna mteremko mkali na kumuona rafiki yake baba yake Bw. Yunus Athumani. Sheikh Yunus Athumani alimuuliza 'Abdu una nini mkononi?' akamuonesha gazeti la Mapenzi ya Mungu. Sheikh Yunus Athumani alikasirika sana na kusema; 'Hivi huyu Abdallah kama anataka kupotea si apotee peke yake? Anataka kuwakokota na watoto kwenye kupotea

Endelea uk. 7

Bustani ya Washairi

SWALATU WAZAKAATI

1 Rabbi wakuabudiwa, Muabudiwa Jalali
Pekee wazingatiwa, hapatikani wa pili
Wewe wakusujudiwa, wakuombwa kula hali
Niwe mtu wa kuswali, kabla ya kuswaliwa.

2 Ilahi Mwenye kujuwa, ni weye mwenye kubuli
Mikono ninainuwa, mikono yote miwili
Mjao naomba duwa, duwa lenyewe ni hili
Niwe mtu wa kuswali, kabla ya kuswaliwa.

3 Swala ya faradhi dawa, pamoja na ya nafali
Kwa khushui na taquwa, swala kitu cha awali
Uzito wa kuelewa, thamani yazidi mali
Niwe mtu wa kuswali, kabla ya kuswaliwa.

4 Nguzo tano tulopewa, za Islam dalili
Ya kwanza tumeambiwa, kumpwekesha Jalali
Natukaunganishiwa, kumkubali Rasuli
Niwe mtu wa kuswali, kabla ya kuswaliwa.

5 Ya pili twafaradhiwa, swala tano tuziswali
Swabaha na Adhuhuri, Alasiri, Magharibi
Aliishau mekuwa, nyakati tano kamili
Niwe mtu wa kuswali, kabla ya kuswaliwa.

6 Swala tano ni ngekewa, ajuwaye jambo hili
Kuiqimu yatakiwa, lakini lo masalali
Kila tukikumbushiwa, wengi wetu hatujali!
Niwe mtu wa kuswali, kabla ya kuswaliwa.

7 Allah naomba kupewa, shauku hamu ya hili
Niwe wa kuzindukiwa, nisibakiye jahili
Niishike sawa sawa, kila kipindi niswali
Niwe mtu wa kuswali, kabla ya kuswaliwa.

8 Piya niwe wa kutowa, kwenye njiyayo Jalali
Hali nitakayokuwa, usinifanye bakhili
Niwe mwepesi kutowa, nisilimatiye mali
Niwe mtu wa kuswali, piya niwe wa kutowa.

9 Ubakhili ni ukiwa, ubakhili udhalili
Kuwa nao sio sawa, kuwa nao si akili
Ni kujinyima utawa, ucha Mungu na fadhili
Niwe mtu wa kuswali, piya niwe wa kutowa.

10 Nilimapo nikipawa, kwa mavuno mbalimbali
Simsimu na kahawa, mpunga, pamba na fili
Korosho nikijaliwa, m inazi na pilipili
Niwe mtu wa kuswali, piya niwe wa kutowa.

11 Vyema nikijaaliwa, mifugo rasilimali
Wanyama wanaoliwa, baqara, mbuzi, jamali
Kondoo na wa mabawa, korongo, tai, kitwili
Niwe mtu wa kuswali, piya niwe wa kutowa.

12 Nipe moyo wa kutowa, zaka swadaka ya mali
Kukumbatiya si sawa, kushikiliya batwili
Naomba kunusuriwa, kwenye mtego wa mali
Niwe mtu wa kuswali, piya niwe wa kutowa.

13 Huko ulikonitowa, nijile hapa kwa hali
Sina nilichochukuwa, kuja nacho kwa ukweli
Vyote ni metunukiwa, mtunuku We Jalali
Niwe mtu wa kuswali, piya niwe wa kutowa.

14 Lazima nitavitowa, kufilisika sijali
Hata viking'ang'aniwa, sitaenda navyo mbali
Kurejesha kwa Mtowa, ninaona afadhali
Niwe mtu wa kuswali, piya niwe wa kutowa.

15 Ya Allah Wakusifiwa, mali ina kiu kali
Mtu kila akipawa, kiuye huwa miali
Huzagaa na ikawa, kwake ni kimulimuli
Niwe mtu wa kuswali, piya niwe wa kutowa.

16 Basi hiki nichopewa, ijapokuwa kalili
Ninaomba kukitowa, kwenye njiyayo Jalali
Kipokee na Jazuwa, nahitaji kweli kweli
Niwe mtu wa kuswali, piya niwe wa kutowa.

Al-Ustadh Khamisi S. S. Wamwera
Kimbangulile – Mbagala Rangi 3
Dar es salaam

WAZAZI WANGU WAWILI

1 Hata uwe na akiba, mamiliyoni ya mali
Fedha aula vikuba, madola na mariyali
Mambo alotenda Baba, na Mama kwetu ni ghali
Atawalipa Jalali, mimi chakuwapa sina.

2 Hata ningewapa mali, malukuki kwa hisaba
Kulipa zao shughuli, bado pungufu ni haba
Malipo hayo kalili, matundu hayataziba
Mimi cha kuwapa sina, Atawalipa Jalali.

3 Ni ghali ya usuhuba, hayarejeshwi kwa mali
Kwa pishi na kwa vibaba, na vazi la siku mbili
Hili shamba la miraba, hili jambo la asili
Atawalipa Jalali, mimi cha kuwapa sina.

4 Wepi walio mithili, ya wazazi mahabuba
Wazazi wangu wawili, wazazi mama na baba
Haangaza siwaoli, pendo lao la katiba
Mimi cha kuwapa sina, Atawalipa Jalali.

5 Huku mama huku baba, hawa si ndumakuwili
Penzi lao la haiba, huba yao ni kamili
Siyo pungufu si haba, ni pendo la kwelikweli
Atawalipa Jalali, mimi cha kuwapa sina.

6 Mengi yaliwakabili, kwa pamoja takriba
Mepesi na ya thaqili, wao yote walibeba
Ili mimi kula h ali, lisiwe la kunikaba
Mimi cha kuwapa sina, Atawalipa Jalali.

7 Walipopata kibaba, kibaba cha maakuli
Wazazi hawakushiba, wazee walijidhili
Hadi mimi nimeshiba, ndipo nao walikuli
Atawalipa Jalali, mimi cha kuwapa sina.

8 Wakihisi homa kali, ninayo imenikaba
Ni usiku hawalali, hao mbio kinibeba
Naletwa hospitali, hapelekwa kwenye twiba
Mimi cha kuwapa sina, Atawalipa Jalali.

9 Wanibusu kwa mahaba, walipoona dalili
Naliya nalubaluba, kwa swauti ya ukali
Anibembeleza baba, mama naye awaswili
Atawalipa Jalali, mimi cha kuwapa sina.

10 Kwenye mikono miwili, nilipepewa kwa sheba
Kisha nyimbo mbalimbali, niliimbiwa na baba
Mama hakustamili, kanitwaa kanibeba
Mimi cha kuwapa sina, Atawalipa Jalali.

11 Wazazi mama na baba, kuwalipa ni halali
Lakini hilo msiba, ni gumu kwa kila hali
Kuwanyanyasa ujuba, kosa kutokuwajali
Atawalipa Jalali, mimi cha kuwapa sina.

12 Ya Allah Dhul Jalali, takuita mara saba
Wazazi wangu wawili, wazazi mama na baba
Waliko huko Wajali, wape pepo ya rutuba
Mimi cha kuwapa sina, Atawalipa Jalali.

13 Waghufiriye dhunuba, walochuma kama mali
Za ulimi na za riba, za matendo mbalimbali
Waepushe na ikaba, waweke kwenye kivuli
Atawalipa Jalali, mimi cha kuwapa sina.

14 Waketi kwenye kivuli, wasiguswe na dharuba
Na ule moto mkali, ubabuao kasaba
Warehemu tasihili, Rabbi mkubali toba
Mimi cha kuwapa sina, Atawalipa Jalali.

15 Na mapengo yao ziba, yale ya njema amali
Walipokoseya toba, pasioneke muhali
Waweke na maswahaba, mawalii wa Jalali
Walipe ewe Jalali, mimi chakuwapa sina.

16 Ya Allah Dhul Jalali, Mhifadhi wa hisaba
Wazazi wangu wawili, walezi mama na baba
Tafadhali tafadhali, waondolee adhaba
Mimi cha kuwapa sina, Atawalipa Jalali.

Al-Ustadh Khamisi S. S. Wamwera
Kimbangulile – Mbagala Rangi 3
Dar es salaam

Jitahidini Kutangaza Ujumbe wa Islam

Kutoka uk. 11

wa Amri zake mwenyewe. Fanya maombi kwa moyo wote na jikite kwayo na wape familia yako na ndugu mafunzo ya aina hiyohiyo na geukia kwa Allah kwa moyo wote kabisa, na hakuna yeyote atakayeteseka atakayefanya kama hivyo. Mgeukie Mungu kabisa kabisa na hutapata dhara lolote. Kama kuna hasara basi ni ukosefu wa imani na ipo haja kwamba mtu aombe kwa Allah Mwenye Enzi na Allah Ataondoa shida zote na atawafanya maadui wakate tamaa na washindwe.

Allah Azifanywe zishindwe hila zote za wapinzani wa Jumuiya ya Ahmadiyya na Awafanye wakate tamaa. Allah Ametufundisha dua katika Qur'ani tukufu ambayo ni lazima isomwe na mtu aisome akiwa ameielewa vyema. Masihi Aliyeahidwa (AS) kuhusiana na dua za ndani ya Qur'ani ametuongoza na jambo hili limesisitizwa kwamba dua tulizofundishwa ndani ya Qur'ani tukufu zimefundishwa kwa lengo hili kwamba wakati mwaminio wa kweli akioimba kwa moyo wote kwa maneno hayo, Allah Atatapokea. Ili usamehewe madhambi yako na ulindwe dhidi ya majanga na madhara ni lazima uweke msisitizo kwenye dua hizi. Kuna dua kwenye Qur'ani tukufu ambayo kwa kawaida huwa tunaisoma wakati wa sala na Masihi Aliyeahidwa (AS) pia ametukumbusha na amevuta fikra zetu kwenye hiyo kwamba ni lazima daima tuisome na iko kama hivi:

Mola wetu tupe mema katika dunia hii na mema katika Akhera, na utuepushe na adhabu ya moto (2:202)

Masihi Aliyeahidwa (AS) anasema kwamba mtu anahitaji vitu viwili ili kupata ustawi binafsi. Kimoja ni kwamba katika maisha haya mafupi matatizo na shida anazokumbana nazo katika maisha haya aepushwe nazo na pili maradhi ya kiroho na matendo ya kishetani ambayo yanampeleka mbali na Mungu akombolewe kwayo na swala la maisha baada ya kifo ni hali hiyohiyo. Kama uzuri wa dunia aupewe mtu basi hilo litamnufaisha katika maisha yajayo na kuhusiana na ulinzi dhidi ya moto anasema kwamba sio moto utakaokuwa Siku ya hukumu tu, bali kuna mioto mingine mingi duniani kama vile mashaka, wasiwasi, masuala ya kifamilia au shida zingine. Hivyo muaminio wa kweli anaomba kwamba aokolewe dhidi ya aina zote za moto.

Na kisha dua hii ya kupata uimara wakati wa mtihani na uimara dhidi ya adui na kupata mapenzi ya Allah tumefundishwa na iko kama ifuatavyo:

Mola wetu, tughofirie dhambi zetu na kupita kwetu kiasi katika mambo yetu: Na uimarishe miguu yetu, na utulinde dhidi ya makafiri" (3:148)

Masihi Aliyeahidwa (AS) anasema kwamba bila shaka kama Allah Asingekuwa ndiye Mwenye kutusamehe basi Asingetufundisha dua hii. Kuna dua ndani ya Qur'ani:

"Mola wangu mimi ni muhitaji wa heri yoyote utakayoniteremshia" (28:25)

Dua hii lazima isomwe mara kwa mara. Kuna dua nyingi zingine ndani ya Qur'ani Tukufu ambazo ni lazima zisomwe ili kupata Rehema kutoka kwa Allah. Kama nilivyosema kwamba Masihi Aliyeahidwa (AS) amesema kuwa Allah Ametaja dua hizi ndani ya Qur'ani tukufu kwa lengo kwamba tuzisome mara kwa mara na kwa moyo wote asaa Allah Atazipokea.

Kisha tuna maombi ya Mtume Mtukufu (SAW) na maombi ya Masihi Aliyeahidwa (AS). Kuhusiana na dua moja Masihi Aliyeahidwa (AS) anasema kwamba hili limefunuliwa kwangu na Allah. Amenifundisha dua hii:

'Rabbe Qulu Shain Khad-e-Mauka, Rabbe faf azni, warsurni, warhamni'

Ee Mola kila kitu kinakutumikia wewe, Ee Mola Utulinde, Utusaidie na Utuhurumie.

Anasema kwamba Allah Ameweka kwenye moyo wangu kwamba hili ni neno la kimuujiza na yeyote atakayeomba dua hii ataepushwa na aina zote za mitihani na shida. Allah Aiwezeshe Jamaat, Jumuiya na kwa ujumla kila mmoja dhidi ya kila aina ya madhara na majaribio yote ya maadui yarudishwe kwao na waweze kusikia wito wa Masihi Aliyeahidwa (AS) uliotumwa na Allah na kwa kuwa Jumuiya moja waweze kuimarisha na kueneza ujumbe wa kweli wa Islam duniani kote.

JALSA SALANA TANZANIA 2016

Amir na Mbashiri Mkuu nchini anapenda kuwaarifu Wanajumuiya wote kwamba, Jalsa Salana ya Kitaifa mwaka huu itafanyika kwenye siku za Ijumaa, Jumamosi na Jumapili tarehe 30, Septemba na 01 na 02 Oktoba 2016, katika eneo la Jumuiya, Kitonga Dar es Salaam. Inshaallah. Hivyo tunatakiwa kuzingatia yafuatayo:

1. Wanajumuiya wote wajitahidi kuhudhuria Jalsa hiyo na ihakikishwe kwamba kusiwepo hata tawi moja katika kila mkoa ambalo halitokuwa na angalau mtu mmoja atakayehudhuria Jalsa.

2. Masheikh na walimu wajitahidi sana kuwakumbusha wanajumiya juu ya umuhimu na baraka za kushiriki kwenye Jalsa Salana kwa nauli zao wenyewe. Pia kwa vile wanajumuiya wa mkoa wa Dar es Salaam kimsingi hawahitaji nauli ikilinganishwa na wale wa mikoa mingine basi wote wasikose kuhudhuria Jalsa hiyo. Mwanajumuiya wa Dar es Salaam ambaye hatohudhuria Jalsa mwaka huu atatakiwa kujieleza baada ya Jalsa kwa nini ameshindwa kuhudhuria.

3. Marais wa mikoa na viongozi wengine wa Majlis za matawi nao wajitahidi kuhudhuria Jalsa Salana kwa nauli zao.

Itumikieni Jumuiya

Kutoka uk. 4

hajalipa michango yake tokea muda fulani. Kama inaulizwa kwamba kama michango hailipwi sasa Wasiya unakaa wapi ndipo unapofanywa uchunguzi inagundulika kuwa halikuwa kosa la mwana Wasia. Amelipa michango yake lakini ofisi haikutunza kumbukumbu kikamilifu.

Kwanza kabisa, ripoti ya aina hiyo inasababisha mashaka kwa mwana Wasia kinyume na haki. Pili, udhaifu wa mfumo wa Jamaat unaacha taswira mbaya. Hivi sasa kuna mpangilio madhubuti wa kimfumo, kuna Kompyuta na hivyo makosa yote ya aina hiyo yasitokee. Makatibu wa Wasia na wa Fedha katika kila nchi wachochee utendaji wa makatibu wa Wasia na wa Fedha wa kila tawi. Hili pia ni jukumu la Amiri kwamba awe ananafanya tathmini ya jambo hili mara kwa mara. Kazi yao sio tu kukusanya michango na kutoa ripoti bali pia ni kazi ya Amiri kuufanya mfumo huu uwe unategemeka na kudumisha mawasiliano thabiti kati ya Markaz na matawi.

Napenda pia kusema jambo fulani kuhusiana na Wabashiri na Walimu. Baadhi ya sehemu mikutano ya mwezi ya Wabashiri na Walimu haifanyiki kwa kudumu. Mbashiri Mkuu anao wajibu wa kuhakikisha kwamba mikutano hii inafanyika kwa kudumu. Kazi za Tabligh na Tarbiyyat lazima zifanyiwe tathmini, mafanikio yanayoonekana lazima yajadiliwe, na wengine wajaribu kufaidika na njia zilizotumika kuleta mafanikio yanayoonekana. Ripoti zitolewe kuhusiana na maagizo ya Makatibu kwenye matawi aidha kutoka kwao wenyewe au kutoka Markaz. Walimu lazima pia waangalie ni kiasi gani cha kazi kilichofanyika katika kila tawi katika suala hili na pale ambapo makatibu hawako hai, hasa hasa kuhusiana na Tabligh, Tarbiyyat na masuala ya Fedha, wabashiri na walimu walitilie maanani suala hilo.

Allah Awape fursa viongozi wote kwamba katika kipindi cha miaka mitatu ijayo Allah Amewapa nafasi ya kuhudumia waweze kuonyesha utendaji wa hali ya juu kabisa wakitumia nguvu zao zote na wawe mfano katika Jumuiya kwa kila neno na tendo. Amin.

Ahmadiyyat Mkoani Kagera

Kutoka uk. 5

huku!!'. Ili kumnusuru Abdu akaingia ndani na kumletea kitabu cha Sheikh Abdallah Salehe Farsiy 'Upotofu wa tafsiri ya Makadiani'. Abdu alikwenda nacho mpaka nyumbani na siku alipokwenda pia kwa Sheikh Hafidh Suleiman alienda nacho. Sheikh Suleiaman alipokiona akatabasamu na kusema; "Kitabu hicho tayari kimeshapata jibu" kwa hiyo akampatia kitabu cha "Uongofu wa Tafsiri ya Qurani Tukufu" kilichoandikwa na Sheikh Kaluta Amri Abedi.

Masheikh waliofika Bukoba wakati huo wa Bw. Abdallah Bishazo ni pamoja na Sheikh Hafidh Suleiman na Sheikh Yusuf A. Kambaulaya kama tulivyokwisha ona hapo juu. Na mwana Jumuiyya mwingine aliyeimarisha Jamaat ya Bukoba ni Bw. Iftikhar Ayyaz ambaye alikuwa ni Afisa wa Elimu mkoani Kagera. Kama tulivyokwisha sema Sheikh Yusuf A. Kambaulaya alikuwa anatumikia mikoa miwili Kagera na Mwanza. Bw. Abdallah Bishazo alimtoa mwanae kuwa Waqf na Sheikh Kambaulaya alimsubiri melini lakini hakuonekana.

Licha ya watoto wa Abdallah Bishazo wapo wanakijiji wa Katoma waliojiunga na Jumuiyya ya Ahmadiyya hao ni pamoja na Zuberi Makwabe, Juma Kaigwa na Habibu. Vitisho vingi vilitokea kwa hao waliojiunga. Moja ya tishio kubwa ni kwamba yeyote anayejiunga na Jumuiyya ya Ahmadiyya asipewe urithi. Hata hivyo Jamaat ya Katoma iliendelea kuwa imara na hata Bw. Abdallah Bishazo alipofariki mwaka 1981 miaka minne baadae Jamaat ya Katoma iliweka jiwe la msingi la Msikiti. Msikiti huu kama ilivyo misikiti mingi ya Ahmadiyya ulipata upinzani mkubwa wakati wa kuujenga. Kila hila zilitumika ili kukwamisha ujenzi wa Msikiti huo. Lakini njama hizo hazikufanikiwa. Moja ya njama iliyotikisha ni ile hoja ya kwamba Msikiti ungelileta usumbufu na kelele kwa ajili ya adhana kwani Msikiti huo ulikuwa unajengwa karibu na Mahakama. Kwa upande wa utetezi Wanajamaat walisema; ilikuwa ni mara ya kwanza wao kusikia kuwa adhana ni kelele. Walitoa mifano ya Tabora ambapo Msikiti upo karibu na Mahakama na hatimae iliamriwa ya kwamba itolewe adhana ili ionekane kama je kweli kuna usumbufu wowote kutokana na adhana? Alitafutwa miongoni mwa wenye sauti kubwa miongoni mwa Wasuni lakini njia za Allah ni nyingi. Ulitokea upepo na sauti ikapeperushwa mbali na hapo hoja ya kelele ya adhana ikapuuzwa. Msikiti umejengwa karibu na mahakama na hakuna usumbufu wowote.

Jamaat ya Katoma ipo mstari wa mbele katika mahubiri. Wamekuwa wakitoa vipeperushi na kuwa na mijadala na Masheikh wa Bukoba. Katika patashika hiyo Masheikh wa Kisunni walitangaza kuwa kwa sababu Waahmadiyya wamepotea watakufa kwa UKIMWI. Hata hivyo historia inashuhudia kuwa ni masheikh hao ndio waliokutana na adhabu hiyo.
Kama tulivyosema utafiti juu ya Ahmadiyya Kagera unaendelea na Inshallah mwenye taarifa yoyote kuhusu Ahmadiyya mkoani Kagera tutaipokea kwa mikono miwili.

Mwisho.

بسم الله الرحمن الرحيم

JUMUIYA YA WAISLAMU WAAHMADIYYA TANZANIA

RATIBA YA MKUTANO WA MWAKA WA 47 TAREHE 30 SEPTEMBA - 02 OKTOBA 2016.

KIKAO CHA KWANZA: IJUMAA JIONI - 30/09/2016		
MUDA	**TUKIO**	**MHUSIKA**
9:00 – 10:00	Kusikiliza hotuba ya Ijumaa ya Khalifa mtukufu a.t.b.a.	Wote
10:00 – 10:10	Usomaji wa Qur'ani Tukufu na Tafsiri (41:27—33)	Hafiz Zafrullah Abdulrahman
10:10 – 10:20	Usomaji wa Shairi:	Mwl. Mohammed Habibu
10:20 – 11:20	**Hotuba ya Ufunguzi wa Jalsa 2016**	Amir Sahib
11:20 – 11:50	***Hotuba ya Mgeni Maalum***	***Mgeni Maalum***
KIKAO CHA PILI: JUMAMOSI ASUBUHI - 01/10/2016		
3:30 – 3:40	Usomaji wa Qur'ani Tukufu na Tafsiri (41:34—40)	Mwanafunzi kutoka Jamia
3:40 – 3:50	Usomaji wa Shairi:	Mwanafunzi kutoka Jamia
3:50 – 4:00	***Kumkaribisha Mgeni Maalum***	***Amir Sahib***
4:00 – 4:30	***Hotuba ya Mgeni Maalum***	***Mgeni Maalum***
4:30 – 5:10	**Mada 1: Mungu Wetu ni Mungu Aliye Hai.**	Sheikh Athumani Kambaulaya
5:10 – 5:50	**Mada 2: Mtukufu Mtume s.a.w. Mfano ulio bora katika maisha ya familia.**	Asif Mahmood Butt
5:50 – 6:00	Usomaji wa Shairi/Qasida	Atfalul Ahmadiyya
6:00 – 6:40	**Mada 3: Jazba ya Masihi Aliyeahidiwa a.s. katika Kufuata Sunna za Mtukufu Mtume s.a.w.**	Sheikh Bakri Abedi Kaluta
6:40 – 9:00	Sala ya Adhuhuri / Alasiri na mapumziko	Wote
KIKAO CHA TATU : JUMAMOSI JIONI - 01/10/2016		
9:00 – 9:10	Usomaji wa Qur'ani Tukufu na tafsiri (41:41—45)	Sheikh Ahmad Daudi
9:10 – 9:20	Usomaji wa Shairi:	Bw. Muhammad Rafiq
9:20 – 9:50	***Hotuba ya Mgeni Maalum***	***Mgeni Maalum***
9:50 – 10:40	***Salamu za wageni waalikwa mbalimbali***	***Wageni waalikwa***
10:40 – 11:20	**Mada 4: Majibu dhidi ya tuhuma kwamba Islam ni Dini inayofundisha fujo.**	Abdulrahman M. Ame
11:20 – 12:00	**Mada 5: Jinsi Mtukufu Mtume s.a.w. alivyowatendea kwa wema wasio Waislam.**	Dr. Kitabu Pazi
KIKAO CHA NNE: JUMAPILI ASUBUHI - 02/10/2016		
3:30 – 3:40	Usomaji wa Qur'ani Tukufu (24:52—58)	Mwl. Ramadhan Shaaban
3:40 – 3:50	Usomaji wa shairi:	Mwl. Chande Nyenje
3:50 – 4:20	***Hotuba ya Mgeni Maalum***	***Mgeni Maalum***
4:20 – 5:00	**Mada 6: Nafasi na Jukumu la kila Muahmadiyya katika ujenzi wa Jamii yenye utangamano.**	Sheikh Abid Mahmood Bhatti
5:00 – 5:40	**Mada 7: Wajibu wetu sambamba na kiapo kitukufu tulichofanya wakati wa maadhimisho ya Karne ya Ukhalifa.**	Sheikh Karimuddin Shams
5:40 – 5:50	Usomaji wa Shairi/Qasida	Nasiratul Ahmadiyya
5:50 – 6:30	**Mada 8: Wajibu wetu juu ya Malezi ya Waahmadiyya wapya.**	Mzee Salum Thani
6:30 – 9:00	Sala ya Adhuhuri / Alasiri na mapumziko	Wote
KIKAO CHA TANO: JUMAPILI JIONI - 02/10/2016		
9:00 – 9:10	Usomaji wa Qur'ani Tukufu (16:121—129)	Fadhluilahi Abdulrahman - Ahmadiyya Secondary
9:10 – 9:20	Usomaji wa Nazm: Urdu	Arish Fozan - Morogoro
9:20 – 9:30	Usomaji wa shairi:	Mwl. Makarani Balama
9:30 – 9:50	***Hotuba ya Mgeni Maalum***	***Mgeni Maalum***
10:20 –	**Utoaji wa zawadi/Hotuba ya Amir Sahib/Kufunga Kikao/Maombi.**	Amir Sahib

Naitafuta Jana kuielewa Leo

Na Mahmood Hamsin Mubiru – Safarini Kagera, Mwanza na Uganda.

Ni dhahiri shahiri na upo ushahidi wa kutosha wa kuthibitisha kuwa Jumuiyya ya Waahmadiyya nchini Tanzania ilisajiliwa rasmi Tabora mwaka 1934 chini ya uongozi wa Mbashiri wa kwanza kutumwa Afrika Mashariki – Maulana Sheikh Mubarak Ahmad (HA). Lakini ni kweli pia kuwa walikuwepo Waahmadiyya wanaofanya kazi katika shirika la reli, walikuwa ni wengi lakini maarufu miongoni mwa hao ni Bw. Fazl na Bw. Hussein Ahmad ambae alifahamika kwa jina la Kanyenyela likiwa na maana ya sauti ndogo. Bw. Kanyenyela baada ya kustaafu shirila la reli aliamua kuweka maskani yake mjini Tabora na akawa Mkandarasi, msambazaji wa kokoto na mchanga wa kujengea. Bw. Kanyenyela pia alishiriki kikamilifu katika ujengaji wa Msikiti wa kwanza kujengwa na Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya nchini Tanzania ujulikanao kama Masjid Fazal. Bw. Kanyenyela hakuwa peke yake bali alijaaliwa kupata watoto ambao pia walitoa mchango mkubwa katika maendeleo ya Ahmadiyya Mjini Tabora. Watoto hao ni pamoja na Mansoor Ahmad, Taimur Ahmad, Zahoor Ahmad na Muzaffar Ahmad.

Historia hiyo ya mwanzo iliyotukuka ya Jumuiyya ya Ahmadiyya inamsukuma mtu kujiuliza swali moja la msingi nalo ni; nani alikuwa mzalendo wa kwanza kujiunga na Ahmadiyya? Unaposoma historia ya Ahmadiyya katika nchi ambapo Ahmadiyya inaendesha mahubiri utakuta historia inayokueleza mzalendo wa kwanza kujiunga na Ahmadiyya. Kwa mathalani nchini Uganda mzalendo wa kwanza kujiunga na Ahmadiyya alikuwa Sheikh Ibrahimu Semfuma. Uelewa wangu huu ulisukuma ghera ya kihistoria ya kutaka nami kujua nani alikuwa na bahati ya kuwa mzalendo wa kwanza kujiunga na Ahmadiyya nchini Tanzania.

Kazi hii hakuwa sahali –rahisi, ilinibidi nitumie njia tatu katika kutegua kitendawili hiki. Kwanza kuwahoji wale waliokula chumvi nyingi, ya pili kupitia nyaraka za zamani zinazopatikana katika nyumba ya nyaraka za taifa iliyopo Dar es salaam na kusoma maendeleo ya historia ya Ahmadiyya kama yalivyoandikwa na wataalamu wa historia maarufu miongoni mwa hao Dr. Earl Martin wa Canada ambaye amepata shahada ya Uzamili (PhD) kwa sababu ya kufanya utafiti juu ya historia ya Ahmadiyya nchini Tanzania.

Kwa kuwasiliana na baadhi ya wazee, usomaji wa nyaraka na vitabu vya historia jina linalojitokeza sana la kuwa mzalendo wa kwanza kujiunga na Jumuiyya ya Ahmadiyya nchini Tanzania ni jina la Bw. Suleiman Kaishozi maarufu kama Kagunju – mfanyabiashara wa kijiji cha Bugombe tarafa ya Kanyigo ambayo kwa hivi sasa ni wilaya ya Misenyi mkoani Kagera.

Kwa ruhusa ya Amir Sahib na Mbashiri Mkuu Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry nilifunga safari ya kuelekea Bukoba na mikoa mingine tarehe 09/07/2016. Kabla ya safari niliwasiliana na Bw. Ismaili Ishengoma wa mjini Dar es salaam na Bw. Abdu Bishazo wa Katoma Bukoba. Wanajamaat hawa wawili wanazo historia zao za kusisimua. Bw. Ismaili Ishengoma ni mtoto wa Bw. Amri Kweyamba mzee maarufu aliyejiunga na Jumuiyya ya Ahmadiyya wakati akisoma shule ya wavulana Tabora. Nae ni mzaliwa wa Bugombe Kanyigo kijiji cha Bw. Suleiman Kagunju. Baada ya kujiunga na Jumuiyya ya Ahmadiyya Bw. Amri Kweyamba alifanya bidii kuwahubiri ndugu zake nao walijiunga na Jumuiyya, hao ni Hassan na Halfan. Kwa kunisaidia katika utafiti Bw. Ismaili Ishengoma alimpigia simu mtoto wa Bw. Halfan aitwaye Mudrikat ili aweze kutusaidia. Na kama tutakavyoona baadae Bw. Mudrikat alitoa siku nzima akitutembeza Kanyigo na kutupeleka mahali muhimu tulipotumaini kupata habari zaidi za Bw. Suleiman Kaishozi Kagunju.

Bw. Abdu Bishazo ni mtoto wa Bw. Abdallah Bishazo aliyezaliwa mwaka 1908 na kufariki mwaka 1981 huyu ni mwana Jumuiyya wa mwanzoni mjini Bukoba aliyefanya kazi kubwa ya mahubiri. Historia ya Ahmadiyya ya Rwanda sawa na Rais wa Ahmadiyya nchini Rwanda Bw. Adam Kahamile tuliyekutana mjini Kampala inatokana na mahubiri ya Bw. Bishazo ambaye alifanikiwa kuwapata vijana hao wa Rwanda akiwemo na Idrisa Sengoga ambao wameisimamisha Jumuiyya ya Ahmadiyya nchini Rwanda na kujenga msikiti. Allah Amemlipa sana Bw. Abdallah Bishazo kwani wanawe ni Wanajamaat nao ni pamoja na Abdu, Omari na Yahya. Bw. Abdu Bishazo aliacha kila kitu na tukashughulikia safari ya kwenda Kanyigo ili kufanya utafiti kuhusu Bw. Suleiman Kaishozi Kagunju ambaye jina lake lilitumiwa na Masuni kuwatisha wote waliokuwa wanataka kujiunga na Jamaat. Kila mara walisema yatatukuta yaliyompata Suleiman Kagunju. Hiyo iliongeza hamu yetu ya kuyamaizi yale yaliyomsibu Suleiman Kagunju. Bw. Abdu Bishazo ni mtu makini na mahiri wa mipango. Tulipokwishaweka kila kitu sawasawa kuwasiliana na Bw. Mudrikat kupata pikipiki, asubuhi ya tarehe 14/07/2016 tulipakizana kwenye pikipiki kuelekea Kanyigu. Ilikuwa ni asubuhi na baridi ya Bukoba ilikuwa imeshika kasi. Tulipita milima na mabonde wakulima wakiwa mashambani. Tulifika Kanyigo kwenye milango ya saa nne asubuhi. Kituo chetu cha kwanza tuliposimama tulimuulizia Bw. Mudrikat na bahati nzuri haikuwa mbali na nyumba yake na hivyo tukafika pale. Tuliteremka taratibu hadi kwa Bw. Mudrikat na tulikuta nyumba imefungwa na hapakuwepo na mtu yeyote pale nyumbani. Mungu bariki haikupita hata dakika tano tukasikia gari inasimama na kushusha mizigo. Kumbe alikuwa ni Bw. Mudrikat aliyekuwa anatoka Bukoba Mjini kununua bidhaa za duka lake. Alitukaribisha ndani tukajitambulisha na akatuambia kuwa alikuwa amekwishapata habari zetu kutoka kwa Bw. Ismail Ishengoma. Alitukaribisha kwa vinywaji na tukamueleza madhumuni ya safari yetu. Yeye binafsi alisema hakuwa anajua mengi kuhusu Bw. Suleiman Kaishozi Kagunju na akatushauri tumuone Alhaji Sheikh Swaibu Yusuf –Sheikh wa mtaa na mjumbe wa jopo la Maulamaa Bukoba. Alhaji Sheikh Swaibu Yusuf alitukaribisha kwa heshima na mapenzi. Tulimueleza shida yetu kuwa tunafanya utafiti kuhusu yule anayeaminiwa kuwa ni Ahmadiyya wa kwanza nchini Tanzania. Sheikh alitutazama na kusema; ningeliweza kuwasaidia kama ningekuwa nafahamu chochote, lakini binafsi sijui lolote kuhusu Suleiman Kaishozi Kagunju. Mimi na Bw. Abdu Bishazo tulitazamana na tulikaa kimya na baadae sote kwa pamoja tukakubaliana kuwa kuna jambo kubwa alilokuwa anaficha na kulionea haya. Hakutaka kuzungumzia chochote na hivyo akaingia katika mada nyingine. Yeye alitueleza kwamba ni msomaji mzuri wa Mapenzi ya Mungu na akatueleza kwamba siku hizi halipatikani. Nilijaribu kutoa utetezi na kumuahidi kuwa tutahakikisha kuwa analipata gazeti naye akatupatia anuani yake ili tuwe tunamtumia gazeti hilo linapotoka. Tukiwa pamoja na mwenyeji wetu Mudrikat tuliagana na Sheikh Swaibu. Taratibu tulianza safari ya kuelekea kwa Bw. Mudrikat. Tulipofika yalipo maduka tuliwaona wazee wawili wamepiga kofia zao nzuri nikapata kishawishi cha kuzungumza nao. Tulisimama tukatoa 'Assalaam Alaikum' waliitikia vizuri na kutukaribisha. Kama tulivyofanya kwa Sheikh Swaibu tukaeleza madhumuni ya safari yetu. Kabla hatujaanza mazungumzo walitaka tujitambulishe. Bw. Abdu Bishazo alijitambulisha na mimi nikaawambia ni Mhariri wa gazeti la Mapenzi ya Mungu. Walitazamana na wakaanza kutoa yao ya moyoni. Nyinyi waandishi mna mambo. Kesho na keshokutwa mtatuweka katika magazeti siku hizi Waislam ni wengi wapo wenye suruali fupi, Bw. Sisi hatuna lolote la kusema. Niliwaeleza taratibu shabaha ya utafiti wetu na kueleza msimamo wa Ahmadiyya katika mambo mengi. Hatimae nikawaambia tutawaandikaje vibaya wakati sisi ni watoto wa hapahapa Bukoba? Hapo wakataka kujua zaidi. Nikawaeleza jina la baba yangu na kaka zangu hapo ndipo imani yao iliporudi na tukaanza mazungumzo. Mzee wa kwanza tuliyezungumza naye ni Bw. Annas Mohammed – Mwanasiasa mashuhuri wa Kanyigo ambaye alimfahamu vilivyo Bw. Suleiman Kaishozi Kagunju. Yeye alikuwa kijana wa makamo wakati Bw. Suleiman alipokuwa anafanya biashara na aliweza kutuonesha alipokuwa anafanyia biashara. Alitueleza kuwa katika safari zake za kibiashara Bw. Suleiman Kagunju alipata mafundisho mapya. Aliyaleta kijijini na yalipingwa kwa nguvu zote. Japo, alisisitiza Bw. Annas Mohammed kwamba, licha ya upinzani huo mkali Bw. Suleiman Kagunju alikuwa anaheshimiwa. Mafundisho aliyoyaleta yaliyowaudhi watu ni kusema Utume unaendelea, Nabii Issa a.s. amefariki, haya yalionekana kuwa ni mambo mapya na ya kuzua na hivyo akatengwa na jamii. Jambo lililowaudhi kuliko yote ni kwamba hao aliowafuata waliopewa jina la Qadiani walikuwa na Kalima yao iliyosema; "Ash-hadu Allaa ilaaha Illallah, wa Ash-hadu Anna Mirza Ghulam Rasuulullah". Alipofika hapo Bw. Abdu Bishazo uzalendo ukamshinda na akamwambia Bw. Annas Mohammed tunashukuru sana Bw. Annas bila shaka na sisi utatusaidia. Kwani Bw. Annasi alisema kwamba anacho kitabu kinachoeleza Kalima hiyo. Ndipo tulipomtaka akatuletee kitabu hicho, lakini aliionekana kutazama juu na pembeni na hatimae kutweta ndipo tulipojua kuwa hakuwa na kitabu chochote kinachoeleza hivyo na hakuwa na ushahidi. Ndipo tukaona tuendelee na mazungumzo yetu.

Bw. Annas Mohammed alisema Bw. Suleiman Kaishozi Kagunju alikuwa ni mfanya biashara na mara kwa mara mwaka 1947 alikuwa anamtuma stempu mjini Bukoba. Alisisitiza kuwa vijana wa kijijini hapo walipenda sana kuwa karibu nae kwani alikuwa mzee mwenye busara aliyewashauri vijana na wazee wawe na khulka njema. Yeye mwenyewe alionesha mfano mwema wa yote aliyoyasema. Chuki ya watu ilikuwa kwa yale aliyoyaleta kutoka Tabora. Vinginevyo alikuwa tegemeo kubwa hapa kijijini.

Mzee wa pili aliyekuwa tayari kuzungumza juu ya Bw. Suleima Kagunju alikuwa ni Bw. Athumani Kassim Kajwagya ambaye kwa miaka mingi alikuwa kondakta wa basi. Yeye alimuona Bw. Suleiman Kagunju na kushuhudia masaibu yote yaliyompata. Bw. Kassim anasema wenyeji wa Kanyigo walitikiswa na mafundisho mapya aliyoyaleta. Wao hawakupenda mabadiliko. Wao walipenda mambo yaendelee kama yalivyokuwa hapo zamani. Upepo wa mabadiliko uliingia maslahi ya watu na kutia mchanga katika kitumbua chao. Hivyo ilizuka dhahama kubwa na upinzani wa hali ya juu. Alitengwa na kuzomewa kila alipopita. Kila alichokigusa kilionekana kuwa kimechafuliwa. Hali ilikuwa ngumu kiasi hiki kwamba hata ndugu zake wa damu pia walimtenga. Lakini yeye hakutetereka. Alisimama imara na kuendelea na mahubiri ya kueneza vitabu na gazeti la Mapenzi ya Mungu. Ubaya wa Bw. Suleiman Kaishozi Kagunju ni kuleta mafundisho mapya. Na kupinga kwa nguvu zake mafundisho yaliyokuwepo. Tulipodadisi iwapo alizikwa na Waislam pindi alipofariki Bw. Kassim alishikwa na kigugumizi. Tuliwashukuru wazee hao tukateremka kwa Bw. Mudrikat na kumshukuru kwa msaada aliotupatia.

Bw. Mudrikat hata hivyo alitushauri tuonane na mtoto wa Bw. Suleiman Kaishozi Kagunju Bi. Jannat ambaye ni Katibu wa CCM mkoa wa Tabora na alitueleza juu ya Amina ambae ni marehemu. Mimi (Muandishi) nilifahamiana na Bi. Amina kwa njia mbili; dada yake wa baba yake mdogo Mama Magera aliolewa na kaka yangu Badru Nsubuga. Binti huyo alisoma Bwiru na hatimaye kuwa Mwalimu. Baba yake alipofariki Sheikh Kaluta Amri Abedi alimlea kabisa kama binti yake. Watoto wa Sheikh Amri hususan wale wakubwa siku zote walimwita dada. Alipata bahati ya kwenda London na kukutana na Khalifatul Masih – IV Hadhrat Mirza Tahir Ahmad (rh).

Utafiti wetu bado unaendelea isipokuwa tumejifunza yafuatayo:-

1. Ni kweli mtu anayeitwa Suleiman Kaishozi Kagunju alikuwepo na aliishi kijiji cha Bugombe Kanyigo.

2. Miaka ya thelathini na tano (35) alileta mafundisho ya Ahmadiyya Bukoba bilkhususi Kanyigo.

3. Anakumbukwa kwa tabia njema na mtu mwenye busara.

4. Alijaaliwa kupata watoto watatu (3) Abdu, Amina na Jannat.

5. Aliendesha mahubiri kwa kusambaza vitabu na gazeti la Mapenzi ya Mungu.

Hatua yetu ya pili katika utafiti wetu nikukutana Inshallah na binti yake Bi. Jannat ambaye kama tulivyokwisha sema ni Katibu wa CCM mkoani Tabora.

Mwisho.

Ziara ya Amir sahib mkoani Shinyanga

Kutoka uk. 12

Inshaallah.

Baada ya hapo Amir sahib alifunua Kitambaa kilichofunika Bango la Ufunguzi kama ishara ya kuufungua Msikiti na akatuongoza kwa maombi ya kimya na baadae sala ya Alasiri ilisaliwa na iliongozwa na Amir sahib mwenyewe, baada ya sala kulikuwa na picha ya pamoja na wanajamaat wa hapo kama ukumbusho , kisha ilifuatia chakula kilichoandaliwa kwa ajili ya sherehe hiyo.

ZIARA NA UFUNGUZI WA MSIKITI WA JAMAAT TAWI LA MWAMALA.

Katiak Tawi hili Amir sahib alifikasiku ya jumatano tar 25/05/2016 saa tano kamili asubuhi na alipokewa na wanajamaat waliojipanga mstari kwa ajili ya kumsalimia na baada ya kusalimiana na wanajamaat hao Amir sahib alielekea msikitini ambapo sherehe za ufunguzi wa msikiti zilianza kwa usomaji wa Qur`an Tukufu pamoja Tafsiri yake iliyosomwa na Mwl Hussein Abeid na baadae alisimama Mwenyekiti wa Kijiji cha Mwamala ndg Charles Yona Ndugulile ambaye alitoa Salamu na shukurani kwa Jamaat kujenga Msikiti katika kijiji chake na kutuomba tujitahidi kuwaelimisha wakazi wa hapa ili wapate mabadiliko, na pia akatumia fursa hiyo kuikaribisha rasmi Jamaat katika kijiji chake. Baadae alisimama Rais wa Jamaat Kanda ya Ziwa ambaye yeye baada ya salaamu alisema kwamba Aliyepo mbele yenu ndie Amir Mkuu wa Jumuiya ya Waislam wa Ahmadiyya Nchini Tanzania na yeye alitumia fursa hii kumkaribisha Amir Sahib ili azungumze na Wanajamaat pamoja na Wananchi kwa ujumla.

Amir sahib alisimama kuwahutubia , baada ya salaam, Tashahud, Tasmia na kusoma surat Fatiha kwanza alitoa shukurani kwa wanajumuiya na wananchi kwa kuhudhuria pia alitumia fursa hiyo kuwakaribisha katika hafla hiyo ya ufunguzi.

Alisema kuwa takribani miezi saba iliyopita nilisikia habari za hapa Mwamala kuwa Wabashiri wetu walifika hapa kuwapatieni ujumbe wa Jamaat nayi muliukubali, lakini kwakuwa Jumuiya ilichelewa kuwaleteni Mwalimu wa kudumu hapa mlichelewa kupata malezi na mafundisho mazuri, lakini hata hivyo kwakuwa jumuiya hii ni ya kimataifa na inao mfumo mmoja ndio maana sasa tumewaleteeni mwalimu wa Jamaat ambaye kabla alikuwa katika tawi la kivulini mkoa wa Arusha. Hivyo tunaimani uwepo wake hapautasaidia sana katika suala la malezi na kuwafundisheni elimu nzuri ya ujumbe huu wa kiislaam. Sasa hapa kilichobaki ni wajibu wenu sasa kumtumia mwalimu huyu kwani hivi sasa mpira upo miguuni penu na kilichobaki ni kufunga goli tu. Kwahiyo jitahidini kumtumia ili mpate mafunzo yatakayowafanyeni mbadilike na kuwa watu wema.

Ndugu zanguni baada ya kujiunga na Jamaat ninyi mmekuwa watu maalumu na hivyo mnatakiwa kupata mabadiliko ya kweli, kwani kama zamani kati yenu kulikuwa kuna mtu anakunywa pombe, anasema uongo, anazini na kufanya matendo mabaya anatakiwa kuachana nayo mara moja mambo ya namna hiyo.

Hapa tumjenga msikiti huu sasa lililobaki ni jukumu lenu kuustawisha vizuri, na namna ya kuustawisha ni kuja kufanya ibada hapa na kuleta watoto wenu na nyinyi wenyewe ili mupatiwe elimu ya Kiroho itakayowapatieni mabadiliko makubwa ya kimaisha hapa dunian na huko akhera pia.

Aidha Amir sahib alieleza kwa kirefu kuhusu jamaat hii na misingi yake na kuwataka watu wote wajitahidi kuifuata misingi hiyo ili wawe wanajamaat wema na wapate mabdiliko ya kweili na watu wawe mashahidi kuwa baada ya kujiunga na jamaat mmebadilika na mmekuwa watu wema.

Baadae Amir sahib ailfunua kitambaa katika bango la ufunguzi kuashiria ufunguzi wa Msikiti na kuongoza maombi ya kimya ambapo watu wote walishiriki.

Baadae adhana ya sala ya Adhuhuriilisomwa na watu waliingia Msikitini na sala ya Adhuhuri iliongozwa na Amir sahib na baada ya sala kililetwa chakula kilichoandaliwa kwa ajili ya wageni waliohudhuria.

ZIARA NA UFUNGUZI WA NYUMBA YA MWLIMU TAWI LA KIDANDA.

Jumatano ya tar 25/06/2016 saa tisa na robo Amir sahib alifika katika tawi la Kidanda na kulakiwa na wanajamaat pamoja na wananchi waliojitokeza kumpokea kiongozi huyu wa Jamaat Nchini na baadae alisalimiana nao na alipomaliza kusalimiana nao ndipo hafla ya ufunguzi wa Nyumba ya Mwalimu ilianza kwa usomaji wa Qur`ani tukufu pamoja natafsiri yake iliyosomwa na Kijana wa tawi hilo ndg Ramadhan Mahona.

Baadae alikaribishwa Mwenyekiti wa Kijiji cha Kidanda ambae pamoja na kutoa salaam na shukurani kwa Jamaat alitumia fursa hiyo kumkaribisha Amir sahib kwa mara ya pili kijijini hapo, pia Mtendaji wa Serikali ya Kijiji hicho naye alisimama na kutoa Salaam na shukurani kwa kupatiwa fursa ya kushirki katika mapokezi na Hafla ya Ufunguzi wa Nyumba ya Mwalimu na pia alitumia fursa hiyo kumkaribisha Amiri sahib kijijini hapo na akamwambia kuwa tumefurahi sana kwa kuja kututembelea tena kijijini kwetu, tunaimani tutapata faida kubwa kwa ziara yako hii.

Hatimaye Amir sahib alisimama ili kuhutubia na kuzungumza na wanajamaat na wananchi kwa ujumla ambapo baada ya salaam na Tashahud, Amir sahib aliwashukuru na kuwakaribisha katika tukio hilo muhimu.

Alisema kuwa Alhamdulillaah nilikuja hapa mwezi July mwaka jana katika ufunguzi wa msikiti huu na tulionana, na baadae tuliamua kwamba sawa na haja Nyumba ya Mwalimu ianze kujengwa na hatimaye imekamilika na ndio maana leo tupo hapa kwa ajili ya kufungua nyumba hiyo, na pia akasema kuwa amekuja hapa ili pia apate fursa ya kuongea machache yatakayowapatieni faida na mafanikio ya Kiroho.

Alhamdulillaah Jamaat yetu ni ya kimataifa na inae kiongozi mmoja ambaye ni Khalifatul Masih na pia Jamaat hii imeenea katika nchi 207 duniani na inamfumo na nidhamu moja ambayo ukienda USA, UK, Ghanan, Sieraleon n.k huko kote utakuta mfumo sawa na uliopo hapa Kidanda na hakuna tofauti yoyote kwakuwa hii ni Jamaat ya kimataifa, na ndio maana wanajamaat popote pale walipo wanatakiwa wawe na picha moja ambayo ni Nidhamu ya Jamaat.

Kama mnakumbuka mwaka mmoja uliopita wabashiri wetu walifika hapa kuwapeni ujumbe waMasih Aliyeahidiwa A.S ambao unawataka muwe wakweli na waaminifuna pia kuwa WachaMungu. Hatukuja hapa kuleta ujumbe wa siasa na wala kufanya biashara, bali tulileta hapa ujumbe wa utawa na UchaMungu. Sasa baada ya kujiunga na Islaam papo hapo mnalazimika kufuata masharti ya uislam kama kusali, kupendana na kuheshimiana pamoja na kujitahidi kufanya matendo mazuri.

Mkumbuke kuwa Jumuiya hii haikuja kuleta Jambo jipya wala kusudio lolote zaidi ya kutukumbusha wajibu wetu na kuturdisha kwenye mafundisho sahihi ya Mtume S.A.W.

Aidah napenda kuwakumbusheni kuwa siku chache zilizopita mlisikia habari za Mauaji ya watu waliokuwa wanasali msikitini, kwakweli hayo sio mafundisho ya Uislam, Islam hairuhusu kumuua mtu bila hatia, yote hayo yanatokea kwa sabau ya kukosa elimu sahihi juu ya mafundisho ya Islaam, na ndio maana tunawataka msome vizuri mafundisho ya Qur`an na Islaam kwa ujumla. Tumeleta Mwalimu hapa kwa ajili ya kuwapatieni fursa ya kupata elimu ya dini, hivyo jitahidini kumtumia ili mpate faida hiyo. Mkipata elimu mtaishi vizuri na mtakuwa na mapenzi kwa wote na mtaishi vizuri na mtakuwa wamoja.

Mkikosa elimu hamtaweza kuyatekeleza hayo yote, bali mtafanya kinyume chake.

Aidha napenda kuwakumbusheni jambo la Muhimu kabisa nalo si lingine bali ni jambo la kupata mabadiliko ya kweli baada ya ninyi kuwa mmejiunga na Jamaat. Kama zamani mlifanya mambo yasiyo faa basi hivi sasa mnatakiwa mjibadilishe na muwe watu wa kuigwa mfano na Jamii inayowazunguukeni.

Mwisho nawashukuru viongozi wa Serikali mliokuja hapa na pia wanajamaat kwa kuacha muda wenu na kuja hapa , Allah Mtukufu Awasidieni. Tanzania ni nchi nzuri na yenye Amani, ujumbe wetu hasa ni ujumbe wa Amanina Upendo na Waahmadiyya wote tunaamini kuwa kuipenda nchi yako ni sehemu ya imani kwahiyo sote tuipende nchi yetu.

Baada ya nasaha hizo za Amiri sala ya Alasiri ilisaliwa ikiongozwa na Amir sahib na baadae aliwaongoza wote kwenye ufunguzi wa nyumba ya Mwalimu tawini hapo na baade aliongoza Maombi ya kimya ya pamoja na kufuatiwa na tukio la upigaji picha ya pamoja kwa ajili ya kumbukumbu, kisha watu walipata chakula kilichoandaliwa na watu wa kidanda kwa ajili ya hafla hiyo.

Baada ya hapo msafara wa Amir sahib uliondoka kijijini hapo kwa ajili ya kurudi mjini kwa ajili ya mapumziko na kujiandaa kwa ajili ya safari ya nyingine kesho yake.

ZIARA YA AMIRI SAHIBU JAMAAT MPYA YA BUTIBU WILAYA YA USHETU.

Alhamisi ya tar 26/5/2016 saa tano na nusu msafara wa Amir sahib uliingia katika tawi jipya la Butibu na alilakiwa na wanajamaat waliojipanga mistari kwa ajili ya kumsalimia. Na baada ya kusalimiana na wanajumuiya hafla rasmi ya kumkaribishaAmir shib ilianzakwa usomaji wa Qur`an Tukufu iliyosomwa na Bw Issa Bunela mwanajamaat wa tawi hilo, baadae alisimama Raisi wa tawi na kusoma risala Fupi iliyoandaliwa na Wanajamaat wa Butibu kwa ajili ya Amir sahib.

Katika risala hiyo walimwambia Amir sahib kuwa; sis wanajamaat wa hapa Butibu tunafuraha kubwa sana kufikiwa na mgeni wetu Amir na Mbashiri mkuu wa jumuiya ya waislam wa Ahmadiyya Tanzania, kwani hapo awali hatukuwahi kutembelewa na kiongozi yeyote wa kiislam, lakini baada ya kujiunga na Jamaat Ahmadiyya Viongozi mbalimbali wa Mkoa na Kanda wametutembelea, na pia waalimu wetu wamekuwa wakitutembelea mara kwa mara, hii ni bahati kwtu. Na leo hii tumetembelewa na kiongozi mkuu wa Jumuiya ya Waislaam wa Ahmadiyya, kwa hali hiyo tunafuraha kubwa sana, karibu mgeni wetu Amiri pamoja na wajumbe uliokuja nao leo hii. Jisikieni mko nyumbani.

Aidha Amir sahib tunakuhakikishia kuwa sisi tumejiunga na Ahmadiyya kwa moyo mkunjufu kabisa na kutokana na mabadiliko tuliyoyaona baada ya kujiunga na Jamaat Ahmadiyya tumepata faida kubwa sana kwa kipindi kifupi. Hivyo ndugu Mgeni rasmi eneo hili tulilopo sasa hivi ni mali ya waislamu wa hapa Butibu ambalo tulilipata kwa nguvu zetu wala hakukuwepo na Taasisi yoyote ya Dini ambayo ilishiriki kwa namna yoyote katika upatikanaji wa eneo hili. Sasa kutokana na hilo ndg Mgeni rasmi kuanzia leo hii eneo hili pamoja na Msikiti wake tumelikabidhi kwa jumuiya ya Waislaam wa Ahmadiyya kwa ajili ya kuendelezwa na kudumisha Uislaam hapa Butibu uliofifia muda mrefu , na hii hapa ni HATI ya Makabidhiano tunakukabidhi.

Kilio chetu sisi Wanajamaat wa Butibu ni kupatiwa Mwalimu wa kuja Kutufundisha elimu ya dini ya kiislaam. Ahsante sana.

Baada ya hapo walimkabidhi hati Amir sahib ya makabidhiano ya msikiti na eneo lake nae aliipokea hati hiyo.

Baade alisimama Mwenyekiti wa kijiji ambae pia ni mwanajamaat wa hapo yeye alisimama kutoa salaam na Shukurani na pia kumthibitishia Amir sahib kuwa hili eneo na Msikiti huu ni mali yao wanajamaat wa hapo na akamuomba asiwe na Khoufu yoyote juu ya hilo.

Baadae alisimama Mh, Diwani wa Kata ya Kinamapula ambayo kijiji cha Butibu kimo ndani yake, naye baada ya kutoa salaam na shukurani kwa uongozi wa Jamaat Butibu kwa kumualika yeye aliwashauri watu wote waliohudhuria kwamba yote watakayoyasikia hapa wanatakiwa wayazingatie na akawaambia kwamba wakimjua Mungu vizuri ndio watapata mafanikio, na akatumia nafasi hiyo kumuomba Amir sahib aufanyie ukarabati msikiti huo.

Baade pia alisimama Mkiti wa kitongoji ambaye yeye baada ya salam na shukurani alisema kwamba ni Jambo la heshima kufikiwa na Ugeni kama huu. Zamani kabla hatukuwa na

Itaendelea toleo lijalo

Jitahidini Kutangaza Ujumbe wa Kweli wa Islam

Kutoka uk. 12

mabasi au watoto, wanawake, wazee, wagonjwa na wanaoabudu katika majengo ya ibada wote hao hairuhusiwi kupatiwa madhara.

Wakati mtukufu mtume (s.a.w) alipokuwa anayatuma majeshi yake kwa ajili ya Jihadi alikuwa akiwapatia maelekezo maalum kwamba watoto, wanawake, wazee, wasafiri, miti na viongozi wa dini kamwe hawatakiwi kuuliwa. Na kila mtu asiyeshika silaha na kwa mazingira yoyote hayuko katika sehemu ya mapigano dhidi ya Waislam hatakiwi kufanyiwa dhara. Hivyo hili sio fundisho la Qurani wala sio fundisho la Mtukufu Mtume (s.a.w). Zaidi halikuhusika na kitendo cha Makhalifa na wasahaba zake. Mungu Mwenye Enzi ameipa dini yetu jina la Islam ambalo linaondolea mbali fikira zote za ugaidi na misimamo mikali. Badala yake inatupa ujumbe wa amani na upatanifu kama ni maana halisi ya neno 'Islam' ambayo yenyewe inatupa amani au kuishi kwa amani.

Watu wanaokuwa wadhalimu na hawaamini mafundisho ya Islam wala hawayafuati hawatapata Baraka za Allah. Wamebuni dini yao na sheria zao. Kwa vyovyote wakati Muislam wa kweli anapoamini na kutaka amani na ulinzi na anafanya maombi, basi atalindwa kutoka katika mambo mabaya na matendo ya uovu.

Allah Amesema kwamba Sala / maombi yanazuia kufanya mambo mabaya na yanayochukiza. Islam inatufundisha tusambaze ujumbe wa amani 'salaam' na tuwapatie ujumbe huu wenye kupendeza watu wengine. Kutoa salaam hakujawekewa mipaka kwamba kuwe kwa waislamu tu. Kwa uhalisia hali ya Pakistani ni tofauti. Sawa na sheria ya nchi ambayo ipo chini ya ushawishi wa viongozi wa dini wamehodhi na wamejimilikisha ruhusa ya waislam tu ndio watatoa salam, na makundi mengine ya watu wachache au Waahmadiyya hawaruhusiwi kufanya hivyo.

Katika kipindi cha Mtukufu Mtume (s.a.w) salaam ilikuwa inatolewa kwa kila mtu bila ya kubagua dini au itikadi. Baadhi ya viwango vilivyotajwa kuhusu Islam ni kwa lengo la kusimamisha amani. Ikiwa utaingia kwa undani na kuangalia katika pembe yoyote na amri na kuijadili dini ya kiislam utaiona kuwa ni dini ya Amani, uvumilivu na matendo mazuri. Haihamasishi ugaidi. Islam inaweza kusambazwa tu duniani kupitia mafundisho yake mazuri na sio kwa mafundisho yaliyobuniwa na watu au viongozi wa dini wenye misimamo mikali. Njia hii inaweza kuonyeshwa na mtu yule tu ambaye amefanywa kuwa Imam wa zama hizi. Haki inaweza kusimamishwa tu na mtu yule ambae ametumwa kusimamisha haki na ametumwa kama mtu sahihi wa kutoa maamuzi. Anaweza kuyapeleka mbele mafundisho ya Islam kwa sababu ni yeye ndiye aliyechaguliwa kwa nafasi hiyo. Sisi Waahmadiyya ni wenye bahati nzuri kwa kuwa tumemwamini Masih na Mahdi wa zama hizi na hivyo tumelindwa na fedheha za dunia hii.

Masih Aliyeahidiwa (a.s) alisema kuwa Islam imegawanya mafundisho yake katika sehemu mbili. Moja ni haki juu ya Allah na kisha haki juu ya watu. Haki juu ya Allah ni kumuamini na kumtii yeye. Wakati haki juu ya watu ni kwamba mtu awe mwenye huruma juu ya watu wengine. Hili pia sio sahihi kuwa mtu aumizwe au ajeruhiwe kwa sababu ya utofauti wa dini. Kumhurumia mtu ni jambo lingine na utofauti wa dini ni jambo lingine. Wale wasioelewa maana ya Jihadi wamefanya kuwa sheria kuteka mali za wasio waaminio.

Masih Aliyeahidiwa (a.s) alisema hadi kunihusu mimi wamesema mali yangu inatakiwa kuporwa. Fatwa hizi na maoni haya yanatolewa hata leo kuwahusu Waahmadiyya. Wametoa fatwa kwamba mali zao zinaweza kuchukuliwa, wake zao wanaweza kuchukuliwa. Wakati ukweli ni huu, mafundisho kama hayo ambayo sio sahihi hayawezi kupatikana katika Islam. Islam ni dini safi na huru. Mfano unaweza kutolewa kama alivyo baba, anapendelea kuwa mkuu wa familia. Vile vile anataka kila mtu katika familia yake ahudumiwe kwa ukarimu. Allah hapendelei watu hawa wauliwe. Islam inasema Allah hana mshirika na wanaadamu wote wapate ujumbe wa amani, mapenzi na huruma. Umoja ni lazima utengenezwe. Haya ndio mafundisho ya Islam ambayo yakifuatwa na waislam, kwa hakika yatasimamisha tena utukufu wa Islam katika dunia hii.

Ni lazima watambue haki ya Allah na haki ya kila mmoja. Ni lazima wasimamishe amani na upendo baina ya watu bila ya kujali utofauti wa dini zao. Badala ya kutumia vitendo vya dhuluma na kuua watu wasio na hatia, wanatakiwa wasambaze mafundisho ya kweli ya Islam. Wanatakiwa kuishinda mioyo ya watu na kuwaleta kwenye njia ya kumkumbuka Allah. Badala ya kupata ghadhabu ya Allah kwa kufanya vitendo vya kidhalimu na kuwadhulumu wanaadamu, wanatakiwa kupata mapenzi ya Allah. Islam inatakiwa ichukuliwe kama mapenzi na huruma inayotoka kwa wazazi. Isiwe chanzo cha uonevu na madhara ambayo yanatoa nafasi zaidi kwa wapinzani wa Islam.

Ikiwa kama hawajizuii katika uovu huo wanaoufanya basi ni lazima wakumbuke kuwa njia na mbinu hizo za kidunia haziwezi kusambaza ujumbe wa Islam katika zama za leo. Sisi Waahmadiyya ni lazima tukumbuke kuwa kila shambulizi linalofanywa kwa jina la Islam na watu hawa ni lazima litufanye sisi tutimize wajibu wetu kwa ghera na shauku kubwa. Tunatakiwa tufanye kazi kuelekea kwenye malengo yetu kwa moyo zaidi kuliko hapo awali.

Baada ya kila tukio linaloleta kashifa katika Islam, ni lazima tuiambie dunia kuwa msingi wa dini yangu ni Amani. Ikiwa miongoni mwa wafuasi wa Islam yupo mmoja ambae anafanya jambo la kuharibu amani na utulivu wa dini basi mtu huyo au jamii hiyo ina jambo lake binafsi au wanataka kupata manufaa binafsi. Hilo sio fundisho la Islam hata kidogo. Wajibu huo upo juu ya waliofanya makosa na dini ya kiislam isilaumiwe katika hilo.

Ni Baraka za Allah kwamba Jumuiya ya Ahmadiyya inafanya kazi kwa bidii sana kufanikisha lengo hili duniani kote na sasa kwa Baraka za Allah athari nzuri inajengeka kwenye vyombo vyote vya habari, ambayo inakubaliwa pia na wahariri wa magazeti mbalimbali. Baada ya mauaji ya kikatili ya padre huko Ufaransa mwandishi mmoja ameandika kwamba tendo hili linavuta fikra kuhusiana na ukweli kwamba vita ya kidini tayari imeshaanza duniani. Kisha yeye mwenyewe anaandika kwamba hata hivyo, hii sio hali halisi. Kwa ukweli hii ni vita iliyoanzishwa na watu ambao kwa kutumia jina la Islam wanajaribu kupata faida na (imeanzishwa) na watu wenye ugonjwa wa akili.

Watu pia wametoa tamko zuri kwamba hakuna shaka hii ni vita ya kimataifa lakini sio vita ya kidini. Kinyume chake hii ni vita ya faida za kibinafsi na ni vita ya wale watu ambao wanataka kufanikisha malengo yao wenyewe. Hii ni kwa sababu hakuna dini inayofundisha dhuluma.

Hata hivyo, sasa majukumu yetu yameongezeka mara nyingi kutokana na kuongezeka kwa dhuluma ambako bila shaka kunazaa kisasi. Ni lazima tueneze ujumbe wa Islam kotekote na kwa kila mtu. Kwa vyovyote vile, kwa upande mmoja hii ndio hali. Kuna baadhi ya watu ambao wameupata ujumbe wetu lakini watu wanajaribu kuupaka matope.

Mtu mmoja ameniandikia kwamba mtu fulani ambaye ameacha Islam kwa kutumia nukuu yangu ameweka ujumbe kwenye twitter na pengine ameweka na picha yangu kwamba Islam ni dini ya amani na Mtume Mtukufu (saw) amekataza dhuluma na ukatili. Lakini kisha ameongezea maoni yake kwenye ujumbe huo kwamba agizo hili si kwa wanawake na watu walioritadi Islam. Kuna baadhi ya watu wanaojitokeza kwa kufanya vitendo vya aina hiyo na hii ni kwa sababu wanataka kuhafifisha athari chanya ambayo tunaijenga wanapoona wengine wakiathirika kwa ujumbe wetu wa amani wa Islam.

Njia hii ambayo inatumika sana siku hizi kama Twitter na Facebook na kwa kutumia njia zingine mbalimbali na inatumiwa na wengi kueneza ujumbe. Lazima tuwe macho dhidi ya watu wa aina hiyo na pia tuyajibu haya. Kuna kazi kubwa ya kufanya ili kufikisha ujumbe wa kweli wa Islam duniani kote. Ingawa utambulisho mzuri umeshafanywa na Jamaat lakini bado hatuwezi kusema kwamba imefanyika kwa kiwango cha kutosha. Kipindi hiki cha upinzani ambao ni upinzani dhidi ya Islam kutoka kwa wasio waislam na kwa upizani dhidi ya Jamaat, katika hali ya aina hii tunapaswa kwenda kwa busara na maelewano. Hakuna shaka kwamba Islam ndiyo ile dini ambayo ni lazima itaenea duniani InshaAllah. Hakuna shaka kwamba kuhuishwa kwa Islam kutatokea kupitia kwa Jamaat Ahmadiyya na wanajumuiya. Hili ndilo ambalo Allah Mwenye Enzi Amelikadiria na Amelikusudia. Lakini ni jukumu letu na wajibu wetu kwamba ni lazima tufanye maombi kwamba mifano hii ya maendeleo ipatikane tukiwa hai na mapungufu yetu na madhaifu na uzembe usituweke mbali na ushindi na mafanikio haya.

Kwa ajili ya msamaha wetu sisi wenyewe na kupata Baraka za Allah tunahitaji kufanya maombi zaidi na zaidi. Maadui wa Islam na hao wanaoitwa wafuasi wa walimu wa dini wako dhidi yetu lakini tunapaswa kuondoa kila aina ya woga katika mawazo yetu na lazima tukamilishe kazi ya Masihi Aliyeahidiwa (a.s.) kwa kufanya kila tunaloweza.

Sasa katika baadhi ya sehemu waandishi wa habari na wapasha habari wanahoji swala hili. Wakati wa ziara ya hivi karibuni huko Sweden swali hili liliulizwa kwamba mnapingwa na wenye imani kali na maisha yenu yako hatarini sasa mtafanyaje kazi zenu. Ingawaje hakuna shaka kwamba hofu hii ipo na wanajumuiya wana hofu hiyohiyo lakini hofu hizi haziwezi kutuzuia kufanya kazi zetu. Hatari hii iko kila mahali na kwa kila mtu. Kama ulivyosema ni hatari kwenu. Hakuna tofauti kati ya MuAhmadiyya na asiye muAhmadiyya. Mtu yeyote ambaye hafanyi kazi sawa na matakwa ya hawa wa imani kali ambao wanafanya kazi ili kufanikisha malengo yao ya kichoyo, na ambaye hakubaliani nao bila shaka yumo hatarini. Lakini waAhmadiyya wanapingwa hata na wazawa au wale wasioitaka Islam. Kwa hiyo tuna hofu kutoka pande zote mbili. Lakini potelea mbali muumini wa kweli hajali mambo haya na yuko imara akijizatiti katika imani. InshaAllah kila muAhmadiyya atabaki kuwa hivyo.

Kwa kuangalia hali ya sasa ilivyo ya dunia, Kila muAhmadiyya anahitaji kulindwa dhidi ya shetani. Kwa hiyo, lazima tuyape maombi umuhimu wa juu sana kuliko, na kujitolea ili tulindwe kwa ujumla kama jumuiya dhidi ya matendo maovu ya watu. Hususan katika siku hizi lazima tuweke mazingatio kwa sababu hali inakuwa mbaya zaidi kwa kila siku iendayo kwa Mungu. Allah Mwenye Enzi Atulinde dhidi ya maovu haya na dhidi ya wale wanaofanya dhuluma kwa kutumia jina la Islam. Kwa kufanya hivyo wanaiaibisha na kuipa Islam jina baya. Allah Awakamate watu hawa na Awaadhibu.

Allah Aondoe mitihani na matatizo yetu yote. Mtume Mtukufu (SAW) alielekeza fikra zetu kwenye maombi. Wakati fulani alisema kwamba mtu ambaye kwake mlango wa maombi umefunguliwa, basi bila shaka kwake mlango wa Baraka pia umefunguliwa. Chochote unachokiomba kutoka kwa Mungu, kati ya vitu vyote hivyo kikubwa kati yao ambacho kinamridhia Allah ni kuwa chini ya Ulinzi wa Allah.

Kisha Mtume Mtukufu (SAW) alisema kwamba dua wakati wa mtihani ambao umeshatokea na pia dhidi ya mtihani ambao uko njiani daima ni yenye faida kubwa. Watumishi wa Allah ni faradhi kwenu kwamba daima mfuate njia ya maombi (dua). Wakati fulani alisema kwamba kwa Allah hakuna chenye heshima zaidi kushinda maombi. Dua ndio tendo lenye heshima kupita matendo yote kwa mtizamo wa Allah.

Mtume Mtukufu (SAW) kuhusiana na swala la kujitolea sadaka alisema kwamba ili mlindwe dhidi ya moto ni lazima daima mtoe sadaka na kutoa sadaka katika njia ya Allah ni faradhi kwa Waislam wote. Masahaba waliuliza kwamba kama mtu hana chochote basi je atoe sadaka gani. Mtume Mtukufu (SAW) alisema kwamba basi ayatekeleze mafundisho ya Islam. Ishini kwa kufuata sharia ya Islam na fanyeni vitu vizuri na jiepusheni na maovu. Hili litakuwa ni sadaka kwa ajili ya mtu huyo awe mwanamume au mwanamke.

Lakini hii haina maana kwamba mtu aelewe kuwa kama akitoa sadaka ya kifedha basi anakuwa hawawajibiki kufanya mambo mema. Na kwa hiyo hajizuii kufanya maovu. Badala yake hali isiwe hivyo. Hii ni Baraka ya Allah Mwenye Enzi kwa watumishi Wake kwamba kama kuna kitu kiko nje ya uwezo wao na kwamba hawana fedha za kutoa sadaka basi kama mtu huyo anafanya vitendo vizuri na anajiepusha na maovu, inachukuliwa kuwa ni sadaka kutoka kwake. Vinginevyo kama hatafanya hivyo na hajizuii maovu basi sadaka yake ya kifedha itakuwa haina maana yoyote kama vile isivyo na maana sala ya kujionyesha ambayo haina uzito wowote na inatupiwa kwenye uso wa anayefanya hivyo. Hali kadhalika sadaka za aina hiyo hazikubaliwi na hazina thamani kwa Allah. Inategemewa kwa mwaminio wa kweli kwamba akitoa sadaka na kufanya maombi kwa Allah basi ajaribu kuishi sawa na maamrisho ya Allah. Sharti hili linapotimizwa basi mtu anakuwa na nafasi ya kupokea Baraka za Allah na anaepushwa na mitihani na matatizo. Kuhusiana na hili Masihi Aliyeahidwa (AS) alisema wakati fulani kwamba sadaka na maombi yanaondoa matatizo. Na kuhusiana na hali ya maombi anasema kwamba ili maombi yakubaliwe ni lazima ya kwamba mtu alete mabadiliko ya taqwa nafsini mwake. Kama hawezi kujizuia na maovu na anavuka mipaka ya Allah Mwenye Enzi basi kunakuwa hakuna faida katika maombi ya mtu huyo. Hivyo tukiwa tumebaki ndani ya mipaka iliyobainishwa na Allah tuweke mazingatio kwenye maombi na sadaka ili tuweze kupata Baraka za Allah.

Masihi Aliyeahidwa (AS) akiwa anavuta fikra zetu kuhusu maombi anasema kwamba siku zote ninaomba lakini nanyi pia mfanye hivyohivyo. Kwamba kadiri mnavyozidi katika maombi na kufanya mema kwa ajili ya kutubu Allah Atawalinda. Kama katika nyumba kuna mtu mmoja anayefanya hivyo, Allah Atawalinda wanafamilia wengine. Alisema kwamba watu wenye imani maalumu, Allah Anawageukia na kuwalinda Yeye Mwenyewe na Allah Mwenye Enzi Hamsaliti mtu mkweli abadan!! Na wala Hamuachi peke yake. Kama watu wote wakimkwamisha hawawezi kumdhuru chochote, Allah ni Mshindi kamili Mwenye nguvu zote. Mtu aliyebarikiwa imani anakuwa chini Yake. Kumbuka Allah ni Mwenye nguvu kushinda mwenye nguvu yeyote na hakuna Anayemshinda kwa nguvu. Allah Ana udhibiti

Endelea uk. 7

The First Muslim Newspaper in Kiswahili Language since 1936

MapenziyaMungu

Dhul Qa'dah 1437 AH | AGOSTI 2016 | Zahoor 1394 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu s.a.w

Imesimuliwa na Hadhrat Mukhnaf bin Salim r.a. aliyesema: Tulikuwa huko katika uwanja wa Arafat pamoja na Mjumbe wa Allah s.a.w. ambapo alisema: Enyi watu, ni juu ya kila wenye nyumba (familia) kuchinja dhabihu (kama ana uwezo) kila mwaka. (*Abu Dawud*)).

Jitahidini Kutangaza Ujumbe wa Kweli wa Islam

Na Mwandishi wetu,

Dar es Salaam

Muhtasari wa hotuba ya Ijumaa ya tarehe 29, Julai 2016 iliyotolewa na Hadhrat Khalifatul Masih V, a.t.b.a. kwenye msikiti wa Baitul-Futuh mjini London, Uingereza.

Huzur Aqdas a.t.b.a. alizungumzia juu ya Kutangaza Ujumbe wa Kweli wa Islam.

Baada ya Salamu, Tashahhud, Taaudh na kusoma Suratul Faatiha, Huzur Aqdas a.t.b.a. alisema:

Hali ya dunia ya sasa inazorota kwa kasi na kwa bahati mbaya sababu iliyo nyuma ya mambo haya ni baadhi ya makundi ya Kiislam. Hata viongozi wa nchi za Islam hawaelewi kwamba wafanyao upinzani dhidi ya uislam wanajaribu kuwanasa katika mtego wao huu. Mambo yanayofanywa kwa jina la Islam na Jihadi hayana uhusiano kabisa na mafundisho ya Islam. Pia dhuluma zinazofanywa na serikali hazina uhusiano na mafundisho ya Islam hata kwa nukta ndogo.

Je ni sehemu gani iliyoandikwa katika Islamu kwamba unaweza kumuua mtu asiye na hatia? Watu hawa wanaotoa taswira za maana potofu ya mafundisho ya Islam sio tu kwa jina la dini yao wanawaua wasio Waislam, lakini pia wanawaua waislam wenzao. Hii inajumuisha kundi kubwa la Waislam wasio na hatia kama vile watoto, wazee, wanawake na wanaume. Nguvu ya waislamu inapungua kwa haraka mno, ambapo hili ndio lengo hasa la maadui wa Islam, wanapenda nchi za kiislam siku zote zisiwe na nguvu za kifedha kamwe au kuwa na Amani na utulivu.

Viongozi wa nchi za Kiislam na viongozi wa dini (ambao wanaungwa mkono nao) hawaelewi mafundisho sahihi ya Islam pia hawahitaji kuyaelewa. Wanamkataa moja kwa moja yule aliyetumwa kuwa Imamu wa zama hizi, yule aliyetumwa sawa na bishara za Mungu Mwenye Enzi na sawa na bishara za Mtukufu Mtume (s.a.w). wanamkataa mtumishi wa Allah ambaye ametumwa katika zama hizi ili kuyatambulisha mafundisho ya Islam katika dunia ya leo.

Matokeo yake ni kama niliyoyataja kwamba Islam ambayo ndio dini ya haki na Amani, wale walio wabebaji wakubwa wa bendera ya ujumbe huu na wanaotoa nasaha juu ya nchi za kiislam kusimamisha Amani (ambalo ndio jukumu kubwa la nchi za kiislam) ndio watu au nchi zinazoharibu Amani sehemu zote za Dunia.

Maangamizi tunayoyaona leo katika kila nchi za kiislam na watu wenye malengo yao binafsi wanaofaidika kutokana na hali hizo za uhasama kikubwa ni kutokana na serikali ambazo zinapendelea matakwa yao binafsi badala ya kufanya kazi kwa ajili ya maendeleo ya watu.

Waislam wanawaua Waislam. Kiwango cha uvumilivu miongoni mwa viongozi wa Kiislam kimepungua. Tukio la mapinduzi lililoshindwa lililotokea katika nchi ya Uturuki halina nafasi sawa na mafundisho ya Islam hata hatua zinazochukuliwa sasa na serikali zimeegemea katika mzizi wa dhuluma. Hatua zinachukuliwa dhidi ya wapinzani wote wa serikali hata kama walihusika kwa kiwango kikubwa katika tukio hilo au hawakuhusika. Hatua hii ya serikali italeta madhara mabaya kwa sasa na kwa baadae. Maadui wa Islam watajaribu vya kutosha kutumia nafasi hiyo.

Nchi zenye nguvu kubwa zinauza silaha na zinajifanya wasuluhishi wa pande zote. Iraq, Libya, Siria n.k. Bado tu viongozi wa Islam hawajatambua jambo hili. Ikiwa hawafuati mafundisho ya Islam na hawaishi kama waislam, basi angalau hekima inahitaji wachukue hatua kwa kufikiri sana na kwa umakini. Wanatakiwa waweke umuhimu katika jambo hili kwamba ni nani anayefaidika kutokana na tofauti zote hizi za waislam na machafuko katika nchi zao. Lakini hawaelewi jambo hili. Hata hivyo sisi hatuhitaji kukata tamaa juu ya kuziombea nchi za kiislam na tunatakiwa kuwaombea Allah awape baraka ya hekima ya kuelewa.

Makundi ya kigaidi katika nchi za Magharibi yanauawa watu wasiokuwa na hatia na wanafanya ukatili uliopitliza unaochafua jina la Islam. Jambo hili linaweza kuwa kweli kwamba, ili hawa maadui wa Islam waikashifu Islam katika nchi za kigeni wanahusika katika kila aina ya ukatili huu ilimuradi tu kulichafua jina la Islam. Nchi hizo kwa nembo ya kutoa huduma na kwa kutumia jina la kuwalinda watu dhidi ya ugaidi wameweza kupata kisingizio cha kutozuiwa katika nchi za kiislam. Ikiwa wana uwelewa na mafundisho ya Islam wangejua kwamba hakuna fundisho hilo la uislam ambalo limeruhusu kuuwa mtu asiye na hatia. Pia hairuhusiwi kuwaua abiria kwenye viwanja vya ndege au katika vituo vya

Endelea uk. 11

Ziara ya Amir sahib pamoja na ufunguzi wa Misikiti minne mkoani Shinyanga

Na Mwandishi wetu
Shinyanga

Kutoka toleo lililopita.

Kumbukeni kuwa kutokana na uamuzi wenu wa kujiunga na Jamaat hii, Sisi kama Uongozi wa Jamaat tuliamua kuchukuwa hatua ya kujenga msikiti hapa kwani ni muhimu ili mpate Mahala pa kufanyia Ibada kwani lengo la kuumbwa kwetu ni kufanya Ibada kama alivysema Allah ndani ya Qur`an tukufu kuwa Wamaa khalaqtul Jinin wal insi illa liyaabuduun yaani Jukumu letu la kuumbwa ni kuja kumwaudu Mungu pekee, na ndio maana tukaamua kwambani wajibu wetu kujenga Msikiti hapa ili mpate Mahala pa kutimiza lengo lenu la kuumbwa kwenu kwa urahisi.

Jumuiya yetu ni Jumuiya ya Kimataifa na inae Kiongozi mmoja Ulimwenguni ambaye tunamwita Khalifa mtukufu, Jamaat hii pia imeenea Duniani katika nchi 207 na sehemu zote hizo Jamaat ina picha moja tu, kitu anachozungumza na kukitenda mtu wa Tanzania ndio kile kile atakachozungumza mtu wa USA , Canada, Nigeria Ghana UK n.k, yaani hakuna tofauti yeyote kwakuwa sote tuna picha moja tu ambayo inasimamiwa na nidhamu ya Ukhalifa, hivyo nanyi mmekuwa familia moja iliyounganishwa na Kiongozi mmoja ambaye ni khalifatul Masih wa Zama.

Picha ya pamoja Amir na Mbashiri Mkuu na msafara wake wanajumuiya baada ya ufunguzi wa msikiti wa Nhumbili

Kumbukeni kuwa Jamaat Ahmadiyya tunadai kuwa tunatekeleza mafundisho yote ya Islaam kama vile Sala, Saumu n.k hivyo ni lazima tujitahidi kutekeleza amri zote hizo kwa vitendo.

Amir sahib aliendelea kusema kuwa, ndugu zangu napenda kuwapeni ujumbe kuhusu Islaam. Islaam maana yake ni Amani, Hivyo Waislaam wanatakiwa kudumisha Amani. Nadahani wengi wenu mlihudhuria pale Katika Mkutano wetu na mlishuhdia Bango moja lililoandikwa Love For All Hatred For None, hiyo ni kauli mbiu ya Jamaat ambayotunatakiwa kuitenda sawa sawa na hiyo ndiyo siri ya mafanikio yote. Imani ni daraja, mtu akisema Laa ilaaha illa llaahu Muhammadu rasuulu llaah hii ni hatua ya kwanza,na ili uingie hatua ya pili unatakiwa uyatamke maneno hayo kupitia moyo wako na pia madai hayo yanatakiwa yathibitishwe kwa vitendo vyetu na huu ndio ukamilifu.

Tunaposema sisi ni wanajamaat basi madai hayo tunatakiwa tuyathibitishe katika matendo yetu ya kila siku. Kwakuwa mmejiunga na Jamaat basi mnalazimika kujibadili ili muwe watu wema kwa vitendo, na mnalazimika pia kusoma ili mpate elimu na hasa Elimu ya Dini

Mwishoni nawakumbusheni kuwa mwezi wa tisa mwishoni kutakuwa na Mkutano wa Jalsa Salana hivyo jiandaeni kwa kuweka Nauli ili muhudhurie kwa wingi zaidi ili mpate mwanga zaidi wa Kiroho

Endelea uk. 10